

UTARATIBU WA KANISA



Ndugu tumeita mkutano huu pamoja hapa usiku huu kwa ajili ya kujua jinsi ya kuliendeleza Kanisa la Mungu aishiye, ambapo tunaamini kuwa sehemu ya Kanisa hili.

² Nataka, kwanza, nataka kusema kuwa katika safari zangu kote ulimwenguni, ni juavyo mimi, hapa ndipo mahali pa rohoni sana ambapo unasikia Roho wa Mungu kuliko mahali pengine pote ni juapo. Nilikuwa na mahali pengine pawili mawazoni palipokuwa hivyo, lakini hata sasa yaonekana kama kwamba hatuoni mahali pale; mojawapo pamekuwa dhehebu, na pale pengine pame—pameanguka.

³ Kwa hivyo niliitwa jana na nili—niliambiwa kuwa ninyi nyote mlitaka mkutano mniulize maswali kuhusu wajibu wenu katika kanisa hili, nami...hiyo ndiyo sababu nipo hapa usiku huu, ni...na ku—kuweka kanisa katika, au kuwaambieni mambo ninayodhani ni muhimu kwa kuliendeleza kanisa hili.

⁴ Ndugu, nina hakika kuwa mwatambua hilo, kama nilivyotaja kuhusu hapa kuwa mahali pa kiroho. Si mahali pakubwa sana ulimwenguni, na si mahali ambapo kuna kuimba kwingi mno, kupiga shangwe kwingi sana, na kupaza sauti sana, au kunena kwingi—kunena kwa lugha, na mengineyo, si hayo, lakini ni ubora wa Roho inayotenda kazi hapa katika Maskani haya. Na, sasa, nataka kumsifu na kumshukuru Ndugu Neville, na—nanyi ndugu hapa, wadhamini, na mashemasi, na msimamizi wa shule ya Jumapili, nanyi nyote, kwa—kwa yale mmefanya katika—katika kusaidia kuyaweka haya hivi. Imekuwa maombi marefu yangu, na hamu yangu, tangu nilipokuwa kijana, kuona kanisa limewekwa katika taratibu na kukaa katika taratibu.

⁵ Sasa, tulipozindua kanisa hili, niliwaambia, “Baadaye kidogo nilikuwa na jambo fulani la kuongea nanyi,” jinsi ya kuweka kitu hiki katika taratibu, jinsi ipasavyo kuliendelezwa. Nanyi mlianza...baada ya kuondoka hapa, tulikuwa na wahudumu na kadhalika. Lakini sasa, Ndugu Neville akiwa tu mgeni kati yetu, akaja miongoni mwetu, nilidhani ni heri Ndugu Neville awe imara katika Imani kabla sijatoa mambo kama ninavyokaribia kufanya sasa. Lakini sasa, baada ya kuona kuwa yeye anaimarika vema katika Imani, na anafahamu Mafundisho, na amekuwa shahidi mwaminifu kwa Kristo na anashikilia yale tunaamini kuwa Kweli, naona wakati umewadia sasa, ingekuwa wakati mzuri, kumwendea katika...na kati yenu wazee na mambo hapa ya kanisa, kuwa mtachukua maagizo haya na kuyakumbuka, hayo ndiyo bora sana ni juayo mimi mbele za Mungu. Ndiposa nawatarajia ninyi kutekeleza mambo haya jinsi

ninavyosema, kwa sababu mtu fulani apaswa kuwa kiongozi hapa. Yawapasa mwe na . . .

⁶ Sasa, sijaribu kuchukua mamlaka au kitu kama hicho, lakini, mwaona, mtu au cho chote kilicho na vichwa viwili, haki—hakijui jinsi ya kuenenda. Mungu hajapata kuwa na vichwa viwili kamwe kwa Kanisa Lake, Yeye hakufanya hivyo kamwe, ni kichwa kimoja. Yeye kila mara alitenda hivyo katika kila kizazi vile tumesoma Maandiko kote, kila mara kuna mtu mmoja ambaye Yeye humshughulikia. Kwa sababu ukiwa na watu wawili, una maoni mawili. Yapasa kuwe na uamuzi mmoja thabiti na wa mwisho, na uamuzi wangu wa mwisho ni Neno, Biblia. Kama mchungaji hapa wa kanisa, uamuzi wangu wa mwisho ni Neno, nami nataka . . . Najua ninyi ni Ndugu, mnanichukua mimi kama uamuzi wenu mkamilifu kwa yale . . . mradi ninamfuata Mungu kama Paulo alivyosema katika Maandiko, “Mnifuate mimi kama ninavyomfuata Kristo.”

⁷ Ndiposa ningewatarajia ninyi ndugu wakati wo wote mnionapo nikienda nje ya Maandiko haya, kunijia binafsi na kuniambia nilipokosea. Sijali kama wewe u mmoja wa wadhamini au . . . au kama wewe u bawabu, haidhuru wewe ni nani, una wajibu kwangu (kama Ndugu katika Kristo) kuniambia ninapokosea kimaandiko. Na kama kuna swali, hebu na tuketi chini na tukalitatie, pamoja.

⁸ Na hiyo ndiyo sababu mmekuja, natumai, kwangu usiku huu, mlinileta humu, ni kwa sababu kuna maswali hapa ambayo yanawatatiza mawazoni juu ya mambo haya niliyo nayo—niliyo nayo hapa. Sasa kumbukeni, ndugu zanguni, sijui . . . hakuna jina lililoandikwa kwa yo yote ya kadi hizi, lakini . . . nayo yameandikwa, nami siwezi . . . sijui nani aliyaandika, lakini ni maswali yaliyo mawazoni mwenu, nami niko hapa kuyajibu vema nijuavyo.

⁹ Basi kumbukeni, Mungu ananitazamia kuona kwamba ninakaa katika Neno. Nami nawatazamieni kuona ya kwamba mnalitekeleza Neno, ona, ona, katika kanisa hili. Na kuliweka likiwa la kiroho, kwa maana, kumbukeni, nguvu zote za—za ufalme wenye giza wa Shetani zitaelekezwa kwenu mnapoanza kukua katika Bwana. Na yawapasa mwe wanajeshi, si askari wapya tu. Ninyi ni askari hodari sasa, na mmefunzwa kupigana. Na Shetani atakuja kati yenu na kuwafanya mbishane ninyi kwa ninyi akiweza. Mkataeni mara moja, ninyi ni ndugu; huyo ni adui. Nasi tuko hapa kuinua beramu katika huu wakati wa Nuru ya Jioni, ambapo, ulimwengu unatiwa giza na ufalme wote wa makanisa unaingia katika Baraza la Makanisa. Na hivi karibuni watajaribu kuweka ubao kwenye mlango huu hapa, “Limefungwa!” Ndiposa itatulazimu kukutanika mahali pengine, kwa sababu bila shaka watafunga makanisa haya hivi karibuni tusipochukua ile chapa ya mnyama. Nasi tunatarajia

kudumu waaminifu kwa Mungu hata kifo kitakapotuweka huru, na hilo ndilo tunalonuia kutenda.

¹⁰ Sasa moja kwa moja hadi kwa...Nami ningeuliza, ya kwamba iwapo mambo hayo yataulizwa wakati wo wote, kwamba ukanda huu uchezwe mbele ya washiriki wa kanisa hili (ona?) kwenye mikutano yenu, au kabla ya mkutano, kabla tu mkutano haujaanza. Chezeni ukanda huu na unene! Na kusanyiko hapa wafahamu kuwa watu hawa wana wajibu kwa Mungu, kama kiapo chao katika kanisa hili, kusaidia kushikilia kanuni hizi. Huenda usikubaliane nao; na nikikuruhusu wewe uliendeleze, sitakubaliana nawe pia. Yatupasa tuwe na asilia ambapo kuna jambo la mwisho. Naam, nijuavyo mimi, nayatoa chini ya Roho Mtakatifu, nikimuruhusu Yeye awe Neno langu la Mwisho. Nanyi basi ukanda huu uwe Neno lenu la Mwisho kwa maswali haya.

Sasa, la kwanza ni:

220. Kanisa litafanyaje juu ya wito wa msaada wa kifedha wa...kwa ajili ya chakula na mavazi? Litende—litende nini, kanisa li—lifanyaje?

¹¹ Sasa twatambua kuwa kanisa linawashughulikia watu wake, kwa washiriki wetu hapa wa kanisa, sisi tunajishughulikia wenyewe mradi tu tuna mahitaji ya kuyatosheleza. Sisi hujishughulikia wenyewe, yaani, washiriki thabiti na waaminifu wa Maskani haya wajao hapa na kushiriki pamoja nasi. Tuna wajibu kwao, kama Ndugu zetu na Dada ambao wamethibitisha kuwa washiriki wa kusanyiko hili.

¹² Sasa, tunajua kuwa kuna mamilioni usiku huu wasio na chakula, wasio na nguo, nasi tungalifurahia kama tungaliweza kulisaidia kundi hilo lote, kufanya kila tuwezacho; lakini kifedha hatuwezi kufanya hilo, hatuwezi kusaidia ulimwengu mzima. Lakini tuna jukumu kwa walio wetu. Nami nafikiri, katika hayo, basi tukiwa na cho chote kilichosalia ambacho mgependa kutoa kwa watu ambao si washiriki hapa wa kanisa hili, kitu fulani ambacho mgetaka kuwapa, sharti hayo yatatuliwe na halmashauri ya mashemasi.

¹³ Mashemasi ndio wa—wanapaswa kukabiliwa na pingamizi hii, au tatizo hili, samahani; kwa sababu katika Biblia ubishi ulipotokea kuhusu vyakula na mavazi, na hadhalika, katika kitabu cha Matendo, waliwaita mitume kuhusu hayo, nao wakasema, “Nendeni katafuteni miongoni mwenu watu saba walioshuhudiwa kuwa wema, na wenye kujawa na Roho Mtakatifu, ili washughulikie mambo haya, kwa sababu sisi tutadumu katika Neno la Mungu na katika kuomba.”

¹⁴ Na si wajibu wa mchungaji kushughulikia...vyakula na kadhalika. Hayo yanapaswa kushughulikiwa na mashemasi. Si wadhamini, afisi ya shemasi ndiyo inayopaswa kufanya haya. Ndiposa hili lapaswa ku-...Kumbukeni katika Biblia,

walikuwa wakiwachangia walio wao, Wayunani na—na Wayahudi, ambapo ubishi ulitokea kwamba mmoja alikuwa anapata kidogo kuliko mwingine, lakini walikuwa watu waliokuwa wameuza mali yao yote na kuitolea kanisa kwa ajili ya msaada, kisha wa—wakagawana kati yao sawa. Na kulikuwa na ubishi mdogo uliozuka, na hiyo ndipo tulipopata mashemasi wetu wa kwanza. Na huo ndio mojawapo wa wajibu wao, ni kufanya hayo.

¹⁵ Nadhani kwamba, kama watu, kwa kuwa ni watu wetu, yatupasa tuwatunze. Na lapaswa kuletwa, lalamiko lo lote, kwa mwenyekiti wa halmashauri ya mashemasi, kisha halmashauri ya mashemasi itakutana, na kuona watakalofanya juu yake. Na mambo yote ambayo ni mavazi na vyakula, na misaada ya kifedha, au cho chote kile, sharti yapitie kwa mashemasi. Ndipo mashemasi, wanapoamua kuwa wana—kuwa wana... kile watafanya kuhusu hilo, basi lipelekwe kwa—kwa mweka hazina kuona kama mweka hazina anaweza kwa wakati huu kulipia kiasi hiki cha pesa, au—au kununua mavazi hayo, au cho chote kile. Lakini ha—halmashauri ya mashemasi ingepaswa kukutana kwa ajili ya hayo, na haiwahusu wadhamini au mchungaji. Ni jambo la shemasi, kwa jumla.

Sasa, ndipo swali nambari mbili:

221. Je, inatosha kusema waziwazi toka mimbarani kuwa lugha na tafsiri zapaswa kufanywa katika mkutano fulani kabla ya ibada? Hilo ndilo swali la pili kwenye kipande hiki cha kijikaratasi nilicho nacho hapa, ambayo ni kadi ndogo.

¹⁶ Sasa, hili linahusu mchungaji hapa, ona. Kwa sababu yeye—yeye, hata hivi, kuhusu mambo ya kiroho, yeye ndiye kiongozi wa hayo. Mashemasi ndio askari kanisani kutunza taratibu na kushughulikia mambo haya, na kuwalisha maskini, na kadhalika. Wadhamini wanasimamia fedha pamoja na mijengo, na hayo ndiyo wapaswa kuyashughulikia. Lakini mchungaji anasimamia u—upande wa kiroho, na hili lingeenda kwako, Ndugu Neville.

¹⁷ Sasa, pale...wakati fulani uliopita wakati taratibu ilipowekwa kanisani. Naamini katika kunena kwa lugha, na kufasiri, na karama zote nzuri za kiroho zinazotolewa na Mungu kanisani. Lakini tunaishi katika siku kama vile ilivyokuwa katika wakati wa Biblia, ambapo makanisa... Sasa, mkimtaazama Paulo, yeye alianzisha kanisa kule Efeso, lile kanisa la Efeso, ambalo lilikuwa kanisa lililoimarika sana. Je, mlitambua hivyo? Twaamini kuwa Paulo, naye alisema hivyo mwenyewe, kuwa yeye alinena katika lugha nyingi, nasi tunajua kuwa yeye alikuwa na karama za lugha. Si zile alizojifunza, lakini zile alizokuwa amepewa kiroho, kwa sababu ya vile anavyosema katika Wakorintho pale. Na ili kuhifadhi wakati, huenda...kufungua Biblia na kuwasomeeni, kwa

sababu ingetufanya tu—tukae hapa kwa muda mrefu sana usiku huu, kwa kuwa sina wakati mwingi sana. Na sasa...lakini ili kwamba mpate kuona waziwazi.

¹⁸ Sasa, Paulo hakuwahi hata wakati mmoja kuwaambia Kanisa la Efeso au Kanisa la Rumi, au mojawayo ya makanisa hayo, kuhusu karama zao za kiroho, jinsi ya kuzitumia. Lakini ilimlazimu kuwazungumzia Wakorintho mara kwa mara kuhusu hilo, kwa sababu wao walizozania hayo wakati wote. Na Paulo alisema, alipokuja kati yao, kama walitambua kama mmoja alikuwa na lugha na mmoja alikuwa na zaburi, naye alimshukuru Bwana kwa ajili ya karama zao zuri na mambo kama hayo. Na kama mkitazama katika sura ya kwanza au ya pili ya Wakorintho, Paulo alikuwa akiwaambia wao, mahali pao, wao walivyokuwa katika Kristo, jinsi yeye...wao walikuwa wamechukua mahali pao katika Kristo.

¹⁹ Ndipo baada ya kuwaambia, basi kama baba yeye akaanza kuwacharaza mjeledi, na akisema, “Nasikia kuna ubishi kati yenu, nami nasikia kuwa mnalewa katika Meza ya Bwana.” Yeye hakuwafanya si Wakristo; nanyi ndugu msifanye hivyo, kuwafanya si Wakristo, lakini ni mienendo yao katika nyumba ya Mungu. Hapo ndipo ilipo.

²⁰ Sasa, ningesema hili, kwamba kama Paulo wa kale alivyosema, ya kuwa, “Mkutanikapo pamoja, kama mmoja ananena, na mwingine afasiri. Asipokuwepo mwenye kufasiri, na anyamaze. Lakini kama kuna mfasiri...”

²¹ Sasa, nimechunguza kanisa hapa, nami nimewaona mkikua, nami nimeona karama nyingi za kiroho zikitenda kazi kati yenu. Hakika, wakati mmoja ilinipasa kumjia Ndugu Neville na neno toka kwa Bwana, kumsahihisha juu ya jambo fulani alilokuwa akifanya.

²² Na kama nina...kama bwana ame-...Roho Mtakatifu amenifanya mwangalizi wa kundi la kondoo, ndipo ni wajibu wangu kuwaambia ninyi kweli. Nami namshukuru sana Ndugu Neville, yeye alitii ile kweli. Naweza tu kulisema jinsi Yeye anavyoniambia.

²³ Sasa, juu ya hili, kwa kuwa nimeshaona kanisa lenu lilikua, na kulichunguza. Na katika kanisa, hivi ndivyo tulivyofanya hapo awali, na hivi ndivyo sisi—sisi tunavyotaka liwe tena.

²⁴ Sasa, usipotazama, watoto wanapo...jambo la kwanza mtoto afanyalo ni kujaribu kunena wakati hawezi kunena. Ona? Yeye hugugumiza mno, na makelele, na—na kadhalika, lakini yeye adhani yeye ana...yeye aweza kunena kuliko mhubiri wakati huo. Vema, tunaona hayo si kwa maisha ya kawaida tu, lakini twapata hayo katika maisha ya kiroho pia. Ni *mdogo*. Na ukijaribu kumsahihisha mtoto huyo na kumchapa kidogo kwa sababu yeye ana “gugumiza” na kujaribu kunena, utamharibu mtoto yule. Ona, na utamwumiza. Basi afadhali umwache mtoto

huyo akue kidogo hata atakapoweza kutamka maneno yake halisi, kisha umwambie *lini*. “Si wakati baba anaponena au wakati mama anaponena.” Lakini iwapo ni wakati unaofaa, mwache awe huru. Je, mwanifahamu? Sasa, mwache yeye anene wakati wake ufikapo wa kunena.

²⁵ Sasa, kama nimeshakuwa na cho chote ambacho kimekuwa mwiba mwilini mwangu, kule nje mikutanoni, ni mtu fulani kuinuka ninaponena kisha anatoa ujumbe kwa lugha na kukatiza Roho. Ndiyo kwanza nitoke kwenye mkutano kule New York na mahali mabalimbali ambapo wahudumu huacha hayo yaendeleo, wakati baada ya wakati, na si kitu ila—ila farakano. Una, Mungu anaposhughulikia upande mmoja wa mawazo, Yeye... ingekuwa—ingekuwa... Yeye angekuwa akivunja kusudi Lake Mwenyewe, kama Yeye anajaribu kukupeeni wazo fulani, kwa kusanyiko, kutoa wito wa madhabahuni kisha kitu fulani kiukumbe.

²⁶ Kwa mfano, hivi. Tunaketi mezani, tukiongea, nasi tunaongea habari za Bwana. Na mtoto akimbie mezani, upesi sana, akatize yale tunayotenda, naye apaze sauti, apige makelele, “Basi! Mama! Wee! Jamani! Nimeingizia timu goli. Kisha tumefanya *hivi, vile, na vinginevyo!*” Nasi tulikuwa tumeingilia somo takatifu sana. Naam, kuingiza goli, hilo ni sawa kwenye mchezo wa mpira wa kibao, hilo ni sawa. Lakini yeye yuko nje ya taratibu anapotukatizia ujumbe tunaозungumzia. Hebu na angoje hata wakati wake uje ndiposa atwambie yale yeye aliyofanya kwenye mchezo wa kibao.

²⁷ Sasa, hayo ndiyo tunayopata kwa karama siku hizi. Hiyo ndiyo sababu Mungu hawezi kuaminisha karama nyingi sana za kiroho kwa watu, hawajui jinsi ya kuvisimamia. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, sababu hatuna zaidi ya tulivyo navyo.

²⁸ Kisha twaona kuna uigaji mwingi wa karama za kiroho. Lakini siamini iko hivyo hapa kanisani mwetu. Nina shukrani kwa ajili yake. Siamini ni kuigiza kamwe. Naamini tuna vipawa halisi, lakini yatupasa tujue jinsi ya kutumia vipawa hivyo.

²⁹ Na ndipo unapoenda kufanya kitu fulani kizuri... Tuseme tu ulikuwa ukimfanyia tajiri wako kazi na ukaanza kazi yako ya kwanza na u tayari kushika amri, ndipo tajiri wako anakuamini naye atazidi kukupandisha cheo wakati wote.

³⁰ Sasa, naamini wakati umefikia maskani ya Branham, kujua yale... kupokea vipawa anavyotupea Mungu, ili Mungu aweze kutuaminisha hata kitu kikuu sana kuliko tulicho nacho. Lakini hatuwezi kuendelea... na unamwona mtu ambaye kila mara sharti amwambie na kila kitu. Basi kumbukeni, “Roho za manabii hutii nabii,” yasema Maandiko. Mnapomwona mwanamume ambaye unapaswa kumsahihisha, au mwanamke, na mtu huyo anatoka nje ya taratibu, halafu unamwambia Kweli ya Maandiko, basi yaonyesha ya kwamba roho iliyo

juu yao si ya Mungu. Kwa sababu Biblia ilisema, “Roho wa manabii,” au, “kutoa unabii,” hiyo inamaanisha kutoa ushuhuda, kuhubiri, kunena kwa lugha, au lo lote lile, kwa sababu lugha zilizofasiriwa ni unabii. Kwa hivyo inamtii nabii, na Neno ni nabii. Kwa hivyo sisi—sisi twaona kuwa si taratibu kwa mwanamume au mwanamke kuruka juu na kutoa ujumbe, haijalishi vipi wanavyotaka kulifanya, hali mhubiri yuko mimbarani.

³¹ Sasa natoa shauri hili kwa Maskani ya Branham, kwa kuwa vipawa vye—vyetu tupatavyo. . . Nasi tuna watu bora sana waliokarimiwa hapa. Sasa, kila moja ya karama hizo ni huduma. Hizo ni karama, kama tu vile kuhubiri ni karama, kama vile uponyaji ulivyo karama, kama vile vitu vingine vilivyo karama, hizi ni karama, zenyewe ni huduma. Na kila mtu ameagizwa kusubiri huduma yake mwenyewe.

³² Kwa hivyo na Maskani ya Branham yaendelezwe hivi, na katika siku ile, hasa siku hizi ambapo tumekuwa na mengi sana (sitaki kusema hili, lakini) kuiga kwingi sana. Hatutaki kuigiza. Hakuna mtu, hakuna mtu mwaminifu anayetaka kuigiza. Sisi. . . Kama hatuwezi kuwa na iliyo halisi, na tusiwe na lo lote kwa vyo vyote vile, hebuni tungoje hadi tupate iliyo halisi. Sasa, naamini ninyi—ninyi watu mngeskubaliana na hilo. Hatutaki cho chote cha kuigiza. Ndugu zanguni, hatuwezi kuanzisha kuiga kitu fulani na kuondoka humu ulimwenguni. Yatupasa tuwe na kile kilicho halisi, na kile kilicho yakini. Kama hatuna, hebu na tungoje, hadi tukipate ndiposa tutanena neno juu yake. Ona?

³³ Sasa, ningesema, acha wanaume hawa na wanawake wanaonena kwa lugha, na kutoa unabii, na kutoa ujumbe. . . Nami—nami naamini pamoja nanyi watu kuwa hizo ni halisi. Sasa, Bibia imesema, “Jaribuni mambo yote, lishikeni lililo jema.” “Kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa, hii ndiyo raha niliyosema kuwa wangeingia,” na mle katika Kitabu cha Isaya.

³⁴ Sasa, natoa shauri hili ili kwamba madhabahu yahudumiwe na kipawa kimoja tu kwa wakati mmoja, maana yaturudisha moja kwa moja tena katika taratibu ya lile ninalojaribu kusema: kama mmoja ananena, hebuni roho wa nabii amtii nabii. Je, mwafahamu. Sasa, hebu wale walio na huduma kwa Mwili wa Kristo. . . Na sasa imesemwa, sasa hebu ifanywe. Acheni wale walio na huduma kwa Mwili wa Kristo wasubiri huduma zao, kwa sababu ni huduma toka kwa Kristo kwa kanisa. Lakini hamwezi nyote mkahudumu kwa wakati mmoja, yapasa iwe mmoja kwa wakati mmoja.

³⁵ Maskani ya Branham yatakuwa hivi. Acheni wale wanaonena kwa lugha, na wale wanaofasiri lugha, na wale wanaotoa unabii utakaotolewa kwa kanisa, wakutanike pamoja

mapema katika . . . kabla mkutano kuanza, na wao wakutanike katika chumba kilichochaguliwa, waisubiri huduma ya Bwana.

³⁶ Kama mchungaji anavyopaswa kufanya mwenyewe kabla yeye hajakuja mbele ya makutano; yeye apaswa kuchukua Biblia, aisome katika utulivu wa chumba chake, katika Roho, na atiwe upako aje akanene mbele ya makutano. Asipofanya hivyo, yeye atafarakanika aondokapo kule nje. (Na kila mwanamume na kila mwanamume aliye na kipawa cha kiroho, aje mbele za Bwana.) Na kwa kuwa mchungaji ana huduma Mmoja, yeye ni nabii; Neno la Kiingereza *mhubiri* maana yake ni “nabii,” huyo ni mwenye kutangaza Neno.

³⁷ Wale walio na huduma ambayo inapaswa kuwa sehemu ya mtu mwingine, kama mmoja kunena kwa lugha na mwingine kufasiri, wao na wanasubiri huduma wao pamoja. Hawawezi kuketi katika chumba cha faragha cha kusomea na kunena kwa lugha kisha aje akamwambie yule mwingine yale aliyosema, kwa sababu ingalimbidi kuwa na lugha pamoja na kufasiri. Ona? Sasa, kama yeye ana hizo, vema kabisa, tunataka kulipokea hivyo. Nasi tunataka kanisa lifaidike kwa karama hizi zilizo kanisani mwetu. Mungu amezituma kwetu, na ni . . . tunataka kanisa letu lifaidike kwa karama hizi za roho. Kwa hivyo hebu mtu anenaye kwa lugha, na yule mwenye kufasiri, na yule mwenye kutabiri, wakusanyike pamoja kabla ka—kanisa kukusanyika. Na wao wakutanike chumbani peke yao, wakisubiri huduma ya Bwana kwa kanisa. Je, imeeleweka?

³⁸ Na ndipo, hivi, kama Ndugu Neville asema . . . Vema, sasa hebu nami . . . Samahani, hebu niseme hivi. Kama Ndugu Collins akinena kwa lugha na ndugu Hickerson afasiri, ndipo wao wana huduma *pamoja* kwa ajili ya kanisa. Sasa, hiyo si huduma ya Ndugu Neville; hiyo ni huduma *yako* kwa kanisa. Natoa huu kama mfano. Ndipo ninyi ndugu yapasa muwe tu na hamu katika kuweka huduma zenu mahali pake katika nyumba ya Mungu kama mchungaji anavyokuwa na hamu kuweka yake, kwa sababu ni muhimu sana kufanya hivyo. Lakini huwezi kufanya hivyo faraghani katika chumba chako mwenyewe, kama *wewe* ukinena na *wewe* unafasiri, sharti mkutanike. Sasa, kutanikeni kanisani, mahali fulani chumbani peke yenu, kwa sababu mna huduma ya upweke. Si huduma waziwazi, ni ya kulisaidia kanisa. Ona? Ni kitu fulani cha kusaidia kanisa, lakini haipaswi kufanywa kati ya kusanyiko lote, ni jinsi tu nitakavyowaambieni itafanywa. Ona? Basi lo lote Ndugu Collins anenalo, na Ndugu Hickerson afasiri, kwa mfano, basi na Ndugu *fulani* ayaandike haya, yalivyo. Ndiposa kama inatoka . . .

³⁹ Sasa, sisi sote tunajua Bwana yuaja, tunafahamu hilo. Na kama Ndugu Neville aliamka kila usiku na kusema, “Tazama, Bwana yuaja! Tazama, Bwana yuaja!” hilo lingekuwa sawa, ona. Lakini yeye asema hayo (mchungaji) jukwaani, kwa kuwa yeye ana Neno kwake. Na kama yeye ni mchungaji,

nabii kwa kanisa... au mchungaji, samahani, yeye apaswa kusoma Neno la Bwana na awaambie yale yaliyoandikwa katika Neno la Bwana kuhusu kuja kwa Bwana, nanyi mnaonywa kwa Hilo. Ingawaje, huduma (kwa kanisa) ambayo hatahusika nayo, ni lugha, kufasiri lugha (ambayo ni unabii), au nabii akinena, hayo ni mambo ambayo hayajaandikwa katika Neno. Yale yaliyoandikwa katika Neno, *yeye* apaswa kuyaleta; lakini yale hayajaandikwa katika Neno, ndiyo *wewe* unayopaswa kumwambia. Kama, kwa mfano, “Mwambie Ndugu Wheeler, BWANA ASEMA HIVI, ‘Kesho, katika shimo lake la changarawe, asiende kule, kwa sababu kuna lori itakayoanguka’” au kitu kama hicho, na yapasa kifanywe. Na umenena naye akafasiri, ndiposa weka hayo jukwaani baada ya huduma yako kwisha. Ule...?... usiku, baada ya kanisa... nyimbo, na kuanza kuimba na kadhalika; kama huduma yako imekwisha basi, hebu nao walete unabii ambao umetolewa.

⁴⁰ Nami sidhani kuwa tuna... Au kama unao, uweke mle ndani. Watu hawa wakutanikapo pamoja, wale walio na hekima waje kwanza. Kwa sababu, mwoana, kama mmoja ananena kwa lugha na kutoa tafsiri kulingana na Maandiko, hayo hayawezi kupokewa isipokuwa ishuhudiwe na watu wawili au watatu, mashahidi wawili au watatu (ona?) sharti washuhudie hayo, kuwa wanaamini kuwa ni Neno la Bwana. Kwa sababu... Na wakati mwingine katika hizi huduma ndogo, kama tu katika hudumu nyingine yo yote, unapata roho ambazo si sahihi; ona, zitaingia mle ndani. Nasi hatutaki hilo. La. Tunataka huduma hizi ziwe tayari kuwekwa wazi iwapo zitakuwa wazi, kwa sababu cho chote cha Mungu kinaweza... usijali juu ya kuziweka wazi, zita—zitastahimili majaribu kama ni za Mungu.

⁴¹ Ni kama mchungaji, kama mtu fulani akimpinga kwa Neno, yeye hapaswi kukasirika, yeye ajua hasa yale anayonena, “Njoo humu.” Ona? Na vile vile huduma hizi nyinginezo, sharti ziwe vivyo hivyo.

⁴² Sasa, kama—kama mtu fulani ananena kwa lugha na kutoa ujumbe... Sasa, watu wengine hunena kwa lugha “wanapojijenga nafsi zao,” Biblia ilisema, wanapata tu raha katika nafsi zao. Watanena kwa lugha, wanajisikia. Nao *kweli* wananena kwa lugha, wao kweli hunena kwa lugha, na ni Roho anayefanya hayo. Lakini kama ni kuketi nje pale kusanyikoni, wakinena kwa lugha, wakijijenga nafsi zao tu, basi haina faida yo yote kwa kanisa; mwanamume yule anayejiijenga nafsi yake, au mwanamke yule, au ye yote anayetenda hayo. Ona?

⁴³ Kunena kwa lugha ni karama ya Mungu ya kujenga, kama Paulo asemavyo katika Maandiko, hiyo ni ya kulijenga kanisa. Kwa hivyo ilipaswa kuwe ujumbe wa moja kwa moja toka kwa Mungu hadi kwa kanisa, nje ya yale yameandikwa humu ndani ya Biblia. Ona? Ni jambo fulani ambalo... .

44 Kama ungeniuliza, “Ndugu Branham, nibatizweje?” Naweza tu kukwambia upesi. Haikupasi kunena kwa lugha kuniambia hilo, imeandikwa papa hapa katika Biblia la kufanya kuhusu hayo. Ona? Hainipasi. . . kuuliza swali lo lote juu ya hilo na eti mtu fulani anene kwa lugha na kukwambia. Ona, hayo yamekwisha andikwa.

45 Lakini ukisema, “Ndugu Branham, nifanyeje, nina uamuzi hapa unipasao kuamua kama yanipasa niende kwa kanisa hili au niende kwa kanisa lingine,” au kitu kama hicho. “Au yanipasa nitende *hili, lile?*” Sasa, hilo sharti litoke kwa Mungu. Ona, Mungu apaswa kutwambia hilo. Lakini sharti lije kupitia huduma nyingine, kwa sababu Neno halisemi “Orman Neville na aondoke katika Maskani ya Branham aende kwa Maskani ya Injili yaliyoko Fort Wayne.” Ona, haisemi hayo katika Neno hapa, ona, kwa hivyo hiyo ndiyo sababu ya kuwepo kwa vipawa hivi.

46 Ni kama mtu akija hapa na kusema, “Unaamini katika uponyaji wa Kiungu?” Tunahubiri hayo, tunayaamini, tunaamini katika kupakwa mafuta.

47 Lakini hapa kuna mtu fulani anayesema yeye, “Hawezi kushinda, itakuwaje?” Ndipo inahitaji Mungu, kupitia kwa lugha, tafsiri, kupitia kwa unabii, au njia fulani ya kuingia katika maisha ya mtu huyo na kutoa kitu hicho ambacho yeye amefanya, na kumwambia kuhusu hilo. Hiyo ni huduma ambayo si ya mchungaji, ni ya karama hizi za huduma, lakini haipaswi kufanywa nje pale katika kusanyiko. Ona?

48 Sasa, hapana wakati hata mmoja ambapo Paulo aliliambia lile—kuliambia kanisa la Efeso cho chote kuhusu hayo, walikuwa katika taratibu, kanisa la Rumi au mojawapo wa hayo makanisa mengine; ila lile kanisa la Korintho, nao hawangeweza wenyewe kuwa. . . Naam, Paulo aliamini katika kunena kwa lugha. Yeye alikuwa na kunena kwa lugha katika kanisa la Efeso, vivyo hivyo kama alivyokuwa nako katika kanisa la Korintho (Ona?), lakini yeye angewaambia Waefeso mambo makuu kuliko kule kunena kwa lugha, kufasiri lugha.

49 Naam, basi mtu akiandika ujumbe ambao umenenwa kwa lugha au kutolewa katika unabii, na kuuweka jukwaani, yapaswa usomwe na mchungaji kabla ibada haijaanza, kuhusu “BWANA ASEMA HIVI” toka kwa watu hawa walionena na kufasiri. Na hayo yakitimia vivyo hivyo jinsi tafsiri ilivyosema, tungeinua mikono yetu na kumshukuru Mungu kwa ajili ya Roho Wake kati yetu. Yasipotimia, msifanye hivyo tena hata huyo pepo ameondolewa kwenu. Mungu hadanganyi, Yeye kila mara ni kweli.

50 Kisha, mwoana, mmekomaa kutosha sasa kutenda kama watu wazima, si watoto (“goo, goo, goo”), sharti muwe na maana fulani kwa kitu fulani.

⁵¹ Hebu kanisa sasa, linapokuja katika taratibu, lifikie taratibu *hii*. Mmoja akitoa unabii... Mmoja akiya kati yenu, mjinga, na mnene kwa lugha, mtakuwa washenzi kwake, yeye hajui yale mnayonena. Ona? Na hakika siku hizi ambapo kuna farakano nyingi sana kuhusu hilo, inazusha kukwazika. Lakini hebu mmoja anene kwa lugha, na mwingine afasiri na atoe ujumbe, na usomwe moja kwa moja hapa jukwaani, kuhusu yale yatakayotendeka, ndipo yakitendeka, utaona yatakayotendeka. Waambie kuwa “Kesho wakati *fulani* au juma lijalo wakati *fulani*, *jambo fulani* litatendeka,” basi hebu yule asiyeamini anayeketi pale asikize hayo na aone yakitabiriwa kabla hayajatendeka. Ndipo watajua ni roho wa namna gani aliye kati yenu, itakuwa ni Roho wa Mungu. Hayo ndiyo Paulo aliyosema, “Ndipo kama mmoja aweza kutabiri na afunue mambo ya siri, si waumini wote wataanguka kifudifudi, au asiyeamini, na kusema, “Mungu yu kati yenu?” Ona? Kwa sababu haiwezi kuwa...

⁵² Lakini sasa hatutaki... “Tulipokuwa watoto,” Paulo alisema, “Nilitenda kama mtoto,” yeye aliwaambia Wakorintho pale, “nilinena kama mtoto.” Yeye alikuwa na nia ya mtoto. “Lakini nilipokuwa mtu mzima, nalitupilia mbali mambo ya kitoto.”

⁵³ Sasa, nawaambieni ninyi nyote, ona. Sasa, miaka michache iliyopita, mlikuwa watoto kwa karama hizi, mkizichezea hapa na pale. Lakini mmekuwa shuleni kwa muda mrefu sana sasa, ni wakati wa kuwa wanaume, msizitumie hizi kwa kuzichezea tu. Hizi karama ni takatifu, ni za Mungu, basi msizichezee. Acheni Mungu azitumie. Hivyo ndivyo huduma yako inavyotakiwa kuwa, na hiyo ndiyo njia ya kuendeleza Maskani ya Branham. Na—na haya yakiswaliwa, wakati wo wote, na ukanda huu usimame kama ushuhuda kwamba hivyo ndivyo inavyopaswa kutendwa katika Maskani ya Branham.

⁵⁴ Akiingia mgeni humu. Kwa sababu mnao wakati wote, kwa sababu haya yakiwa maskani yasiyo ya kidhehebu, kuna watu wanaoingia ambao hawajapata haya mafundisho bora, hawana, hawajui vinginevyo. Na mchungaji wao binafsi, wataruka juu na kuharibu ujumbe wake, na kuharibu wito wa madhabahuni, na kunena kwa lugha na kila kitu hivyo. Ninyi ni watu waliofunzwa vema kuliko hivyo. Ona? Ndipo baada ya ibada, yeye akiwa mkorofi, basi ni kazi shemasi kuwaendea. Msimruhusu mchungaji wenu ayafanye hayo isipokuwa hamna shemasi hapa, lakini shemasi ndiye anapaswa kushughulikia hayo. Ona?

⁵⁵ Sasa, baada ya ibada...kama mtu yule akiinuka tu na kutoa ujumbe, mchungaji akitaka kukoma kwa dakika moja hivi kisha aendele, vema, ona, hayo ni juu ya mchungaji. Lakini hebu shemasi papo hapo, kabla mtu yule hajaondoka jengoni, awapeleke kando na aongee nao kuhusu hayo. Na

kama wanaliswali, walete kwenye ukanda huu msemi, “Hili ndilo askofu au msimamizi wa kanisa . . .” Ambaye ni *askofu* . . . msimamizi ye yote. Ona, hivyo ndivyo inavyoitwa katika Biblia, “uaskofu,” ona, kwa hivyo huyo ni msimamizi wa mambo yote ya kanisa. Hebu . . . “Hizi ndizo taratibu na jinsi kanisa letu lifanyavyo. Sasa, tungetaka mje mtoe ujumbe wenu. Lakini kama mna ujumbe toka kwa Bwana na ni . . . na utolewe, njooni hapa muuweke jukwaani na mhudumu wetu atawasomea waumini, ujumbe kwa waumini hawa.” Lakini sharti usiwe tu wa kurudiarudia Maandiko, na mambo kama hayo. Sharti uwe ujumbe wa moja kwa moja kwa watu, wa jambo fulani lililo karibu kutendeka, au jambo fulani liwapasalo kufanya. Je, imeeleweka? Vema.

222. Sasa, kuna njia yo yote bora ya kudumisha taratibu kanisani kuliko kuendelea kuwakumbusha kwa kurudiwarudiwa na mashemasi vilivyo? La, hilo, nimeeleza hilo hivi sasa. Hilo ni swali nambari tatu.

⁵⁶ Mashemasi, kazi yenu ni kudumisha taratibu kanisani, kwa wema na upole, kisha inawapasa, kama mtu fulani akienda nje ya taratibu kanisani, au aingie ndani humu kama mlevi au mtu fulani aingie.

⁵⁷ Kama vile walimpiga mhudumu yule risasi jukwaani usiku mwingine kule. Mlisikia hayo, huyo mlevi aliingia na bunduki yenye mitutu miwili. Yeye alimwita mkewe kwa sauti kuu na—na alimtaka mkewe, naye akamwendea mchungaji. Basi mchungaji akamwonyesha mkewe aliyeketi pale, lakini yeye alikuwa yuaenda kumpiga risasi kanisani, naye mchungaji yule akaanza kumshughulikia. Na badala ya—badala ya . . . Mtu yule—yule aliyekuwa na ile bunduki yenye mitutu miwili akageuka na kumpiga risasi mchungaji akiwa mimbarani, kisha akampiga risasi mkewe, halafu akajipiga risasi mwenyewe.

⁵⁸ Sasa, kama kungekuwa na kundi la mashemasi pale wakati mtu yule alipoingia mlangoni akiwa na bunduki hiyo, wangemshika mikono na kumnyang’anya bunduki ile, Ona? Ona, hiyo—hiyo ndiyo taratibu ya mashemasi. Na sasa, mambo haya yamekuwa jinsi yalivyo sasa na huenda mkatarajia cho chote. Lakini, kumbukeni, mashemasi ni askari wa Mungu katika nyumba ya Mungu, haijalishi anavyowazia mtu ye yote. Wakati mwingine askari hataki kuenda na kumshika mtu fulani, labda mmoja wa marafiki zake, lakini yeye ameapishwa kwa ajili ya kazi fulani, hana budi kutenda hayo haidhuru. Huo ni wajibu wake kwa mji wake. Ona?

⁵⁹ Huo ndio wajibu wa shemasi kwa kanisa. Na kama mtu fulani akiruka juu na kuanza kumkatiza mchungaji, au kitu kama hicho, na mchungaji yumo katika ujumbe wake, mashemasi wanaposwa kumwendea mtu huyo, wawili au watatu wao, waseme, “Je, twaweza kuongea nawe, ndugu?” Ona?

Mwondoeni kanisani, mkamwingize afisini, ndani *humu* au katika afisi nyingine, mkamzungumzie kuhusu hili, mkisema, “Haupaswi kuukatiza.” Unajua, ni—ni faini kubwa kwa sheria kukatiza ibada haidhuru. Ona? Lakini watu fulani, kama mtu mwenye wazimu ama ye yote yule, wanakuja miongoni mwenu, mwajua, na—na wakithiri dini fulani, na—na kuanza kufanya yasiyofaa, basi mashemasi...Na kama yaonekana kama kwamba mashemasi hawawezi kulizuia, ndipo halmashauri ya wadhamini au mtu ye yote yule kanisani aweza kusimama na kumsaidia mtu kama huyo. Mwajua hilo.

⁶⁰ Ba—basi sasa hebu niulize swali hilo hapa tena.

Je, kunayo njia bora ya kudumisha utaratibu kanisani kuliko kuwakumbusha watu kwa kurudiwa-rudiwa na mashemasi?

⁶¹ Sasa, mara kwa mara. Sasa, nafikiri kuwa m—mchungaji, mara kwa mara...Au chezeni ukanda huu, hiyo iwe kama ushuhuda. Mashemasi ni askari, na neno lao ni sheria na taratibu. Ona? Nao wana mamlaka toka kwa kanisa na hata toka kwa sheria za taifa kufanya hiyo nyumba Mungu kuwa mahali pazuri. Na mtu ye yote asiyekubaliana na shemasi hivyo, anapasiwa ki—kifungu cha miaka miwili hadi kumi gerezani. Ukiwaambia waende na wasifanye hivyo, au kitu kama hicho, mtu fulani asiye na adabu, yeye hajui yale anayofanya ku... Yeye anajipasisha mwenyewe, anajipasisha nafsi yake kila aina ya faini, cho chote.

⁶² Na ndipo ifikiapo mahali ambapo mtu fulani...Sasa, kama...Na kama mtu fulani anaruka juu akawa nje ya utaratibu...Labda anene tu kwa lugha au kitu fulani, singelijali na hilo. Ona, acha waendeleo, kwa sababu wao ni wageni. Kama ni watu wetu, basi hebu...Usiku unaofuata, ninyi mashemasi chukueni tu ukanda huu, na kusema, “Sasa, tutasikiza ukanda wa taratibu za kanisa kabla hatujaanza ibada, nataka kila mtu auafhamu.” Nanyi wachungaji na kadhalika mwaweza kufanya kazi pamoja hivyo.

223. Sasa, Ndugu Branham, na shule ya Jumapili je? Ndugu Branham, kuhusu shule ya jumapili (vema), yapasa iwe kabla ya ibada ya mahubiri?

⁶³ Naam, sisi tumekuwa tukifanya hivyo kila mara. Kufanya shule ya Jumapili kabla ibada ya mahubiri. Na hiyo inatoa nafasi kwa watoto wadogo wanaohudhuria shule ya Jumapili, kumaliza masomo yao. Na kama—na kama wao wanataka...na watoto wadogo hawayafahamu, nao watapaswa kuketi wakati wote wa ibada ya mahubiri ndiposa wafanye shule ya Jumapili, hao watoto wadogo wanachoka. Hebuni shule ya Jumapili ifanywe kwanza, muwe na wakati uliowekwa, wakati mmoja uliowekwa ambapo shule ya jumapili itaanza. Msimamizi wa shule ya Jumapili apaswa kutekeleza hilo, aone kwamba shule

ya Jumapili inaanza wakati fulani, wakati uliopangwa. Na inamalizika wakati fulani. Shule zote za Jumapili zimekubaliwa wakati fulani kwa hayo, na ndipo zinamalizika.

224. Je, yapasa mwalimu wa darasa la watu wazima awe mtu mwingine mbali na mchungaji?

⁶⁴ Kama imekubaliwa hivyo. Kama mchungaji ataka kufundisha shule ya Jumapili kisha atoe ujumbe wake baadaye, hilo ni barabara kabisa akitaka kuchukua ibada mbili. Lakini kama hataki, basi muwe na mwalimu wenu wa shule ya watu wazima (ona?) kwa darasa lenu la watu wazima. Kisha iwapo—iwapo mchungaji ana mtu mwingine pale mawazoni, na mtu huyo anataka kufanya hivyo, jipeni dakika thelathini, au wakati wo wote mtakaomkubaliana kwa ajili ya shule yenu ya Jumapili, dakika thelathini au thelathini na tano, arobaini, au wo wakati wote ule.

⁶⁵ Na yapasa kengele iwekwe hapa. Na kengele hiyo ipigwapo, hiyo yamaanisha . . . au kengele ya kanisa, inapolia kule nje, hiyo ni ya kumaliza shule ya Jumapili. Basi kengele hiyo ikilia, hiyo yamaanisha kila kitu kinakuwa kwa taratibu papo hapo.

⁶⁶ Kuwe na wakati kiasi fulani kwa wimbo mmoja au mbili, zo zote mtakazo kuimba. Si wakati mwingi sana, mtawachosha watu kwa kuwakawisha sana, ona. Pigeni tu kengele, muwe na wimbo mmoja na lo lote mtakalotenda, ndiposa myapeleke madarasa yenu mahali pao. Na mara tu wakati huo ufikapo, tuseme utakuwa saa n—nne, au saa nne na nusu, au saa nne na robo, wo wote ule, pigeni kengele na kila mwalimu amalize darasa lake, waje humu kwenye kusanyiko. Halafu . . . Kisha mtoe ripoti ya shule ya Jumapili, kisha mmalize jambo lote, mwache wale wote wanaotaka kubaki kwa ajili ya ibada ya mahubiri wafuate. Ona, ndipo liko katika taratibu.

Swali? **Mangapi . . .** [mtu fulani amwuliza Ndugu Branham, **“Ndipo kwa maneno mengine tuna madarasa mbali mbali.”—Mh.]**

⁶⁷ Ee, naam, yapasa mwe nayo. M—mtoto wa miaka mitatu hawezi kufahamu yale mtoto wa miaka kumi na minne aweza kufahamu. Nadhani nina hilo baadaye:

225. Yapasa kuwe na madarasa mangapi?

⁶⁸ Yapasa mpange madarasa yenu katika . . . Watoto wadogo sana wanaotaka kufundishwa kwa mapicha, hayo hayamfai mvulana au msichana wa miaka kumi na minne. Ona? Yapasa mwe na mtu fulani ashughulikie darasa la watoto wachanga, mama fulani mzee au mtu fulani anayejua kuwatunza hao. Madarasa mengine, nadhani, yapaswa yawe na mtu ambaye aweza sana kutoa Neno. Ona? Na yapasa kuwe na madarasa. Tuseme sasa, kungekuwa na darasa la kuanzia . . . Ikiwezekana madarasa matatu.

⁶⁹ Sharti kuwe na darasa la watoto wachanga, sharti kuwa na wenye umri wa miaka kama mitano hivi. Na wengine wote walio chini ya huo yapaswa wakae na mama zao, na wapelekwa kwenye chumba cha watoto wachanga kama ni lazima katika wakati huo wa—wa mahubiri, wakianza kufanya yasiyofaa. Hiyo ndiyo sababu kuna chumba cha watoto wachanga pale.

⁷⁰ Nami nafikiri kuwa ma—madarasa yapaswa kupangwa toka ya watoto wadogo wenye umri upatao miaka mitano au umri wa miaka sita hadi minane au tisa, kumi, kitu kama hicho. Ndiposa toka umri wa miaka kumi na kuendelea hadi kumi na mitano yapasa wawe katika darasa la—la vijana wa kubalehe. Ndiposa darasa la watu wazima liwe la wanaozidi miaka kumi na mitano, kwa sababu wao. . . kama ni wakubwa kutosha ku—ku. . . siku hizi wanaweza kupata kazi nao wanataka kupiga kura katika umri huo, karibu huo; kwa hivyo wao—wao wanaweza kusikia Neno, lakini waingie katika jumba la hotuba na kupata hayo.

226. Nani wapaswao kuwa walimu?

⁷¹ Naam, hiyo ni juu yenu kupigia kura walimu wenu. Na yapasa mfanye hayo, wawekeneni ndani mle, mchukueni mtu fulani. Kisha kutanikeni pamoja na kanisa, msemi, “Nani. . . Nani hapa anayejisikia anaongozwa na Bwana?” Kisha mtafuteni mwalimu anayestahili. Basi ifanywe hivyo. Yapasa liwe jambo muhimu sana, ndugu zanguni. Kama yule mwalimu hafai, basi wabadilisheni walimu.

⁷² Wakati ufikapo, chini ya Mungu, kama najisikia kuwa Orman Neville hafai kuwa mchungaji hapa, nitalitajia kanisa. Nionapo jambo moja hapa, nikiwazia kuwa ninyi mashemasi hamstahili kuwa mashemasi, nitaliambia kanisa, kuwa “Naona kuna shemasi fulani hapa anafanya jambo asilopaswa kufanya, na yeye hatimizi wajibu wake,” na kadhalika, au mdhamini au ye yote yule. Siwezi kumpigia kura au kutokumpigia, kanisa lapaswa kufanya hayo, lakini hakika nitalinena mbele ya kanisa. Ona, kwa sababu hilo ndilo nipaswalo kufanya. Hivyo ndivyo nipaswavyo kuwa kama msimamizi, ninapaswa kutazama na kuona yale yanayoendelea. Sisi tunaenda Mbinguni, si nje hapa mahali fulani au kuzozana au kitu fulani au kufanya mzaha mwingi wa kukwazana, na kucheza mpira wa kibao. Sisi tuko hapa tukiwa na kitu chenye fadhili mno kilichoko duniani, Neno la Mungu, na lapaswa litendwe kwa taratibu ya Kiungu.

Nani wapaswao kuwa walimu?

⁷³ Naam, hilo ni juu yenu kuwachagua. Lakini ningechukua, kwa watoto wachanga, ningemchukua mama mzee. Baadhi yao wawezao kufanya hilo. Lakini kwa vijana, ningemchukua mwalimu ambaye ni mkali, na si wa kuenda tu nje hapa na kuchoma nyama. Hilo lingekuwa zuri kama wanataka kuenda kuchoma nyama, lakini weka tu jambo lote kwenye. . . Liweke katika Neno, mchagueni mtu anayeweza kushika Neno. Na

itakuwa, kanisa hili haliungi mkono ku- . . . Kuchoma nyama ni kuzuri, na—na mandari mnayotaka kuenda pamoja na kufanya ushirika, hilo ni zuri, hilo ni zuri, hilo—hilo ndilo mpaswalo kufanya kuwafurahisha watoto. Lakini katika mahali *hapa*, hili ni Neno la Mungu. Kuchoma nyama ni mkutanikapo, au kitu kama hicho, lakini si katika hii nyumba ya Mungu. Na jueni haya, hakika twajua hatuamini katika upuzi huu hapa wa—wa—wa karamu na vitu kama hivyo hapa, sisi—sisi . . . mwajua vema kuliko hayo.

227. Nani anapaswa kusimamia shule ya Jumapili na kuiweka katika utaratibu?

⁷⁴ Msimamizi wa shule ya Jumapili. Na hiyo ndiyo kazi yake. Yeye hapaswi kuwa na uhusiano wo wote na mashemasi, wadhamini, wachungaji, ye yote yule, yeye ana afisi yake mwenyewe. Ye yote aliye mwalimu wenu wa shule ya Jumapili, simjui. Lakini huyo mwalimu wa shule ya Jumapili apaswa kuona kuwa kila darasa liko katika mahali pake, na kila mwalimu yupo, au kuweka mwalimu mwingine mahali pa mwalimu huyo kama hawako siku hiyo.

⁷⁵ Ndipo kabla tu ya Jumapili . . . Ma—masomo yanapoendelea, msimamizi wa shule ya Jumapili apaswa kwenda kuchukua sadaka waliyotoa ndani mle (sadaka ya shule ya Jumapili), na ripoti ya wangapi waliohudhuria, walikuwa na Biblia ngapi katika darasa hili, na mengineyo, na kutoa taarifa ya hayo. Kisha asimame mbele ya waumini kabla tu ibada ya mahubiri, anapopewa nafasi kufanya hilo, wanapokuwa na taarifa ya shule ya Jumapili baada ya shule ya Jumapili kwisha, aeleeza waalimu wangapi, wangapi waliohudhuria, na jumla ya waliohudhuria shule ya Jumapili, jumla ya sadaka yote—yote, na mambo kama hayo. Mashemasi, wadhamini, wachungaji, hawapaswi kufanya hayo. Hawana uhusiano na hayo, hiyo ni kazi ya msimamizi wa shule ya Jumapili.

⁷⁶ Ndiposa yeye akiona kuwa shule ya Jumapili yahitaji vitu fulani, basi anapaswa kupeleka hayo kwa—kwa halmashauri ya wadhamini, na wadhamini wanakutanikia hayo, kwanza. Ndiposa wadhamini, wakiona kuwa kuna fedha za kutosha na kadhalika, kupitia kwa mweka hazina, basi hivyo vinaweza kununuliwa; kama yeye ataka vitabu, au cho chote kile, au Biblia au kitu fulani, wanataka kumnunulia mtu fulani Biblia, mwajua, anayeweza kupata maneno mengi sana au kukariri Maandiko mengi sana, zawadi au kitu fulani watakachotoa hivyo, zawadi, nao wanataka kanisa linunue. Basi hayo na yapelekwe kwa—kwa—kwa mashemasi . . . kisha nao waone kama—kama—kama ziko katika hazina. Ona?

⁷⁷ Basi nafikiri hilo linashughulikia hayo maswali matano yanayohusu hilo.

Sasa linalofuata, ni:

228. Ndugu Branham, kuhusu taratibu za kanisa, tumejaribu kuenenda vilivyo jinsi tulivyozifahamu taratibu zilizotolewa wakati wa kuzinduliwa kwa kanisa jipya. Na kwa kufanya hivyo, wengine wametukasirikia sana na kuondoka kanisani. Na wengine hawatasikiza lo lote tusemalo, hasa watoto. Tumeongea na hao wazazi juu ya watoto wao, nao hawatawashughulikia. Sasa, je, tumekosa kufahamu? Au, je, tunaendeleza hayo vibaya? Asante.

Sasa hebu nilijibu hili jinsi linavyoendelea:

Kuhusu taratibu ya kanisa, tumejaribu kuenenda vilivyo jinsi tulivyozifahamu hizo zilizotolewa wakati wa kuzinduliwa kwa kanisa jipya.

⁷⁸ Sasa, hilo ni sawa, mnafanya ipasavyo. Naam, hawa hapana budi ni mashemasi, nafikiri, kwa sababu liko papa hapa kwa kazi ya shemasi. Vema.

Na kwa kufanya hivyo, sisi kila mara . . . watu mara nyingi wametukasirikia. Sana.

⁷⁹ Wao hunikasirikia mimi, pia! Watamfanyia hivyo mtu ye yote. Ona? Mtu afanyaye hivyo, ana kasoro. Hawako sahihi mbele za Mungu, maana Roho wa Kristo hutii mafundisho ya Kristo, nyumbani mwa Kristo, taratibu za Kristo. Ona? Na mwanamume ye yote ambaye . . . au mwanamke, au watu wo wote, watoto, ambao wangemkasirikia shemasi mcha Mungu ambaye angewaambia wao . . . na, au mzazi ye yote ambaye angemkasirikia shemasi . . . Hakika, tunamtaka kila mtu kanisani tuwezaye kumpata; lakini kama hilo lingelela tu shida mahali pengine, kuna mwiba au “sungura katika fungu la kuni,” kama tulivyokuwa tukisema. Mtu huyo ana walakin.

⁸⁰ Wakiondoka, kuna jambo moja pekee la kufanya: acha waende, na waombeeni. Ona? Ndipo labda baadhi ya mashemasi waende kwa kanisa lao . . . au waende manyumbani mwao wakati mwingine, na wachunguze sababu gani waliondoka, na wawaulize ilikuwaje. Ndipo, na kama wao . . . Waone kama wanaweza kuwapatanisha. Iwapo hamwezi, basi chukueni mashahidi wawili watatu pamoja naye, kusudi wafahamike. Ndipo kama hawawezi kufahamika, basi inasemwa mbele ya kanisa kama hao ni washiriki hapa wa kanisa hili. Ndipo wana . . .

⁸¹ Basi kama hao si washiriki wa kanisa hili, maana wao si washiriki wa kusanyiko hili, yapasa *wahimizwe* kutii. Ona, wa—wanapaswa kutii taratibu zetu hapa, kwa sababu hizi ni taratibu za kanisa. Haya ndiyo mambo ambayo hatutaki kuyafanya, mambo ambayo sipendi kufanya, lakini ni mambo yanayopaswa kufanywa. Nami najidhihirisha mwenyewe kwa kuyasema hapa kwa kanda hii, ni mimi. Wanaweza kusikia nikiyanena na kujua ni mimi, si ninyi watu. Mmeniuliza *mimi* maswali haya, nami nawajibuni kadiri nijuavyo toka kwa Neno la Mungu.

⁸² “Sasa, watu hao wakikasirika na kuondoka kwenu, Maandiko yasemaje kuhusu hilo Ndugu Branham?”

⁸³ “Walitoka kwetu kwa sababu hawakuwa wa kwetu.” Na hilo latosha. “Waliacha kanisa,” hivyo ndivyo walivyofanya. Vema.

Wengine hawatasikia lo lote tunalosema, hasa watoto.

⁸⁴ Watoto wanapaswa kuwa na adabu, yapasa waipate nyumbani. Lakini hata kama ni wangu, watoto wangu waingie humu wakati wote, wawe nje ya taratibu, sitaki mfanye upendeleo; Sara, Rebeka, Joseph, Billy, au ye yote yule. Mniambie, nitalitekeleza. Kama hawawezi kuwa na adabu, basi hawatakuja kanisani hadi wapate adabu. Huu si uwanja wa tamasha, hii ni nyumpa ya Mungu. Hapa si mahali pa kuchezea, na kutelezea, na kuandika maandishi, na kucheka, na kusumbuliana, hii ni nyumba ya Mungu, na yapaswa iendelezwe kiungu.

⁸⁵ Mnakuja hapa kuabudu, si hata kutembeleana. Hapa si—hapa si uwanja wa mandari, hapa si mahali pa kutembeleana; hapa ni mahali pa kuzuriwa na Roho Mtakatifu, kusikiza yale anayosema, si ninyi kwa ninyi. Hatuji hapa ku—kushiriki sisi kwa sisi, tunakuja hapa kushiriki pamoja na Kristo. Hii ni nyumba ya ibada. Na watoto yapaswa wawe na adabu njema, na kama wana- . . . ya wazazi wao. Na ijulikane! Iwapo hawa wazazi wa watoto hawatasikiza yale wasemayo mashemasi hawa, basi wazazi hawa wanapaswa kusahihishwa.

Tumeongea na hao wazazi kuhusu watoto wao, nao hawatawashughulikia.

⁸⁶ Kama wao ni washiriki wa kanisa hili, basi yapasa mchukue wawili au watatu pamoja nanyi na mwite huyo mzazi katika mkutano wa faragha, katika mojawapo wa afisi. Sijali ni nani, kama ni mimi, kama ni Ndugu Neville, kama ni Billy Paul na mvulana wake mdogo, kama ni Ndugu Collins na mojawapo wa watoto wake, au wengine wenu. Sisi tuna- . . . tunapendana, lakini tuna wajibu kwa Mungu na Neno hili. Kama ni Dok, haijalishi ni nani, yatupasa tuitane sisi kwa sisi. Mungu awezaje kutushughulikia, kama sisi si waaminifu sisi kwa sisi? Tunawezaje kuwa waaminifu Kwake Yeye? Ona?

⁸⁷ Hili ni agizo, inatupasa tuweke nyumba ya Mungu! Na mashemasi wanahitajika kujua jinsi ya kufanya hilo. Ona? Na hiyo ndiyo sababu ninawaambieni sasa kushikilia mambo hayo. Na kama ni hivyo, unawaambia wazazi nao hatawasikia haya, hawatasikia hilo, basi wewe chukua shemasi mwingine au mmoja wa wadhamini, au au mtu mzuri wa kanisa hili, ukawaite. . . chukua mdha- . . . Chukua halmashauri yenu ya wadhamini, mashemasi wenu wote pamoja, useme, “Ndugu Juma, Ndugu Henderson, Ndugu Jackson,” au ye yote yule, “watoto wao hawana adabu, nasi tumewaambia mara mbili tatu kuhusu watoto wao nao hawasikii.”

⁸⁸ Ndipo mumwite Ndugu Juma aingie au Ndugu *Awaye Yote* mkamwambie, “Ndugu Juma, tumekuita wewe hapa kwa mkutano. Tunakupenda, nasi . . . wewe ni sehemu yetu, wewe ni mmoja wetu. Hebu nicheze tu huu ukanda nawe utasikia yale Ndugu Branham alisema kuhusu hili, ona. Sasa, tumekwambia uwafundishe watoto hao adabu njema. Ona? Kama hawawezi kuwa na adabu njema, nawe huwezi kuwafanya wawe na adabu njema kanisani, waachie mtu fulani unapokuja kanisani hata watakapojua jinsi ya kuenenda katika nyumba ya Mungu.” Ona? Lakini hili ni agizo, sharti lifuatwe! Ona?

Sasa swali lingine laendelea:

Sasa, tumekosa kufahamu?

⁸⁹ La, bwana. Hamjakosa kufahamu, hilo ni sahihi. Ninalisema tena, yale maangizo. Jeshini, hawakuulizi, “*Je*, utafanya jambo fulani?” Kama wewe uko jeshini, *unalazimishwa* kufanya. Ona? Na hivyo ndivyo ilivyo katika . . . Nimelazimishwa kuhubiri Injili. Nimelazimishwa kusimamia Hii haijalishi mtu mwingine na ndugu na wengineo wasemavyo kuihusu, nimeamriwa kufanya hivyo. Sina budi kuwaudhi na kuwachoma watu mioyo, lakini kama nina . . .

⁹⁰ Usitake kuwa kama Oswald. Ona? Kama huwezi kutokubaliana na mtu na kadhalika, kisha usalimiane naye kwa mkono na uwe na kujisikia kule kule kwake, basi una kasoro. Kama siwezi kutokubaliana na mtu (kwa uchungu, toka upande mmoja hadi mwingine) na bado umwazie kama—kama vile Kristo angelifanya, basi kuna kasoro rohoni mwako, sina Roho wa Kristo. Ona?

⁹¹ Kama yeye asema, “Vema, Ndugu Branham, ni—ninaamini kuwa mafundisho yako ni *hivi, hivyo*.”

⁹² “Vema, Ndugu, na tuje pamoja tusemezane, wewe na mimi. Tatalitua sisi wenyewe. Tutaenda hapa chumbani sisi wenyewe, tuhojiane.” Naye ananiudhi tu, na yanipasa nimtupie maneno. Kama moyoni mwangu siwezi kujisikia vivyo hivyo kumhusu, kuwa “yeye bado ni Ndugu yangu nami ninajaribu kumsaidia,” basi sitamsaidia kamwe, siwezi kumsaidia. Kama simpendi, ya nini kwenda kule? Nimwambie, “Kwanza, Ndugu, sikupendi, na hebu niondoe hilo moyoni mwangu papa hapa kabla hatujaingia mle ndani, kwa sababu siwezi kukusaidia hadi nikupende.”

⁹³ Na hiyo ni kweli, na hiyo ndiyo njia. Ona, liendeleze, mumefanya barabara hasa, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Hamkukosa kulifahamu kamwe.

Au je, tunaendeleza hayo vibaya?

⁹⁴ La, ndiyo njia sahihi ya kutenda hilo. Hebuni taratibu izingatiwe! Kwa sababu kila mara ni . . . Sasa, watoto wadogo na kina mama, watoto wachanga na wengineo, wata—watalia,

na wakianza kulia sana na kumsumbua mchungaji wenu pale, kumbukeni, ninyi ni walinzi wake, ninyi mu walinzi wake wa Injili. Ona? Na kama inakatiza ujumbe wa Bwana, ninyi ni mashemasi, mtafanyaje? Ni kama tu mtu akinena kwa lugha, yeye ana wajibu. Na mtu anapohubiri, yeye ana wajibu kwa Neno, yeye ana wajibu kwa mambo haya. Kila mmoja wenu ana wajibu kwa afisi fulani, na hilo ni—na hayo ndiyo tu—tuko hapa kutekeleza.

⁹⁵ Sasa, hatutaki kungoja sana, nami najua nina mapatano ya kukutana katika dakika chache, kwa hivyo nita—nitajaribu kuharakisha upesi niwezavyo.

229. Ndugu Branham . . . Kuna maswali matatu, maswali mawili katika kadi hii hapa. Ndugu Branham, nini maongozi ya kuwatolea watu matoleo kanisani? Hili lifanyweje?

⁹⁶ Nafikiri kuwatolea watu matoleo kanisani hakupaswi kufanywa isipokuwa iwe ni kwa ajili ya mchungaji wenu. Nami nadhani kama mtu fulani akija kwa msaada, au kitu kama hicho. . . Au mtu fulani katika—katika shida mbaya, kama ni mmoja wa washiriki wetu hapa au waumini, tuseme kama ni mmoja wa Ndugu zetu, nao walikuwa na shida fulani; vema, nafikiri basi yapasa hilo litangazwe jukwaani, na hebuni mchungaji afanye hilo, nafikiri ni wajibu wake kufanya hivyo; ndugu fulani aliye na mahitaji ya jambo fulani, acha yeye ayalette kanisani, kama inatakiwa ichukuliwe hivyo.

⁹⁷ Kama ni mtu aliye na haja ha—harafu hamtaki kumtolea matoleo mtu huyo ambaye ni mhitaji, basi acha halmashauri zikutanike na zikubaliane juu ya kiasi fulani kinachohitajika kutolewa kwa mtu huyu toka kwenye hazina. Lakini kama hazina ni kidogo wakati huo nao hawawezi kufanya hilo, basi yapasa utolewe, vema, hebu—hebu. . . hebu ijadiliwe na halmashauri, wakimwagiza mchungaji, basi mchungaji na aulize hili jambo. Kasema, “Sasa, usiku huu, Ndugu yetu Juma alipatwa na—na ajali mbaya mno, nyumba yake ilitেকে. Na usiku huu, kama Wakristo, tutaenda pamoja, kila mmoja wetu atoe ahadi ya kile anachoweza kufanya kumsaidia Ndugu Juma apate nyumba yake tena.” Ona, au—au cho chote kile. Ona, tu—tutafanya hilo. Hebuni hilo lisemwe toka jukwaani, hivyo ndivyo ipasavyo. Ndiposa acha ahadi zitolewe, ndipo mpeni mweka hazina wa kanisa. Na ahadi hizi zilipiwe kupitia kwa mweka hazina wa kanisa, kisha awape. Na mpee kila mtu risiti ya hizo, kwa sababu sijui kama hizo zinalipiwa kodi au la; nakisia ni za kitu kama hicho.

⁹⁸ Naam, Basi iwapo—mgeni akiingia, mgeni aingie kama kwamba. . . Mtu aje na aseme, “Vema mwajuaje? Ni—ni—nilikuwa safarini halafu gurudumu li—likapasuka, nami nataka gurudumu mpya. Nitoleeni matoleo usiku wa leo nipate gurudumu mpya.” Sasa, hilo halipaswi kutendwa. La, hilo

halipaswi kutendwa. Na kama laonekana kuwa—laonekana jambo linalostahili, la mtu mnayemjua, halmashauri ingekutana na kukadiria kiasi fulani cha pesa kwa mweka hazina kumnunulia mtu yule gurudumu au cho chote kile. Au ikiwa hazina ya kanisa imepungua sana na inaamuriwa na halmashauri kuwa hizi . . . Mchungaji hapaswi kuwa na uhusiano wo wote katika hili, ma—mashemasi wanapaswa kufanya hili, ona, au halmashauri hizo. Na kama hili . . . Kama imekubalika, basi mpeni, mchungaji anaweza kukusanya sadaka. Lakini, tazama, kama ni mgeni, ni jambo la haraka, mtu yule anahitaji pesa kidogo nanyi mnaona kuwa kuna sababu muhimi, (sasa haya ni maoni yangu), kama kuna sababu muhimu nanyi mnajua ni za sababu muhimi . . .

⁹⁹ Sasa, kwanza, mkienda juu pale na mtazame vitabu vyangu nyumbani, vya watu wanaokuja na kusema, “Mimi ni Mchungaji *Fulani* toka kanisa *fulani* nami na-nami nilipata shida fulani barabarani hapa, na ni—ninahitaji magurudumu mawili,” nami nilijua kuwa nililingia tu toka mkutanoni na nikachukua sadaka, au cho chote kile, ningempa, karibu nifanye hivyo, kupata magurudumu mawili. Nami natazama orodhani, hamna mhudumu kama huyo, aliyewahi kuishi mahali pale. Na kuna dolla elfu kumi au ishirini vitabuni kwa miaka hii ambayo nimetoa hivyo, sikuwahi kujua lo lote kuwahusu walikokuwa. Hatimaye nikaona, wahudumu wengine wanasema, “Naam, alinidhania kuwa *fulani wa fulani*.”

¹⁰⁰ Sasa, kanisa halihusiki, ila kwa walio wake. Naam. Walio wake, ndio linalowashughulikia.

¹⁰¹ Lakini kama inaonekana kuwa ni jambo muhimu, na ndipo kama ninyi—kama ninyi wadhamini huenda mkasema, “Vema, sasa ngoja kidogo. Mtu huyu, ndilo lile *pale* gari lake, hilo ni lake (ilitendeka), na *hii*. Si wa kusanyiko letu, ona, lakini imetendeka.” Basi kama wanataka kufanya hivyo, na wangesema jambo fulani maalum kuhusu yule mgeni . . .

¹⁰² Si wetu, sasa, ona, si watu wetu, watu wetu wanashughulikiwa hapa kati ya—watu wao wenyewe, Ndugu zao hapa, ona.

¹⁰³ Lakini kama ni mtu fulani toka nje, na mtu yule aseme yeye ana njaa au . . . na mtu fulani anataka kutia mkono mfukoni mwake na ampe msaada, hilo ni juu yako, lakini naongea kuhusu toka kwa kanisa. Ndiposa kama watu wa kanisa *wanaulizwa* kuchanga, basi . . .

¹⁰⁴ Sasa, kama mna mwinjilisti, bila shaka, ndani humu anayehubiri, basi mnachukua . . . mna- . . . hilo lafahamika kabla hajaja, mwajua, ya kwamba mtamtolea sadaka, au mumlipe mshahara, au cho chote anachotaka kufanya.

¹⁰⁵ Lakini basi kama mtu huyu yuko hapa, na ana sababu muhimu, na mchungaji . . . na halmashauri ingetaka kukubali

na kumwambia mchungaji kulihusu, basi acha mchungaji aseme, “Mtu *fulani* anayeketi humu, hatumjui mtu huyo, yeye alikuja akatuomba...yeye asema watoto wake wana njaa. Hatuna wakati wa...hatuna wakati wa ku—ku—ku—ku—kuchunguza madai haya.” Ona?

¹⁰⁶ Kama kuna jambo lo lote kama hilo, basi—basi...kama kuna jambo lo lote kati watu wetu, mashemasi wetu waende kuchunguza madai hayo. Ona? Ndiposa kama yanastahili, basi fanyeni vile. Kama hayastahili, msiyatekeleze, si lazima. Lakini sasa kama ni mtu hapa, mna—mna—mnaacha mchungaji aseme, “Sasa, halamshauri ya wadhamini iliniambia hawakumjua mtu huyu. Lakini mtu huyu anaketi hapa, yeye asema jina lake ni Jim Juma,” au lo lote lile, “naye anaketi papa hapa. Waweza kusimama, Bw Juma? Sasa Bw. Juma, ibada itakapokwisha simama pale nyuma ya mlango mnapotoka.’ Na kama watu wo wote mnajisikia mioyoni mwenu, au lo lote mnalotaka kumfanyia mtu huyu, mpeni mnapoondoka.” Je, hilo limeeleweka, sasa?

¹⁰⁷ Je, ukanda...Na mmoja wa...Ndugu Collins aliyakosa kwenye ukanda wake. Nataka kuyatilia mkazo maneno hayo niliyotaja tena kama...kwa sababu yeye ni mmoja wa mashemasi.

¹⁰⁸ Kama—kama kuna ye yote wa hawa, mtu mmoja aingie ambaye ninyi...na ana jambo la haraka naye anataka matoleo toka kwa kanisa, basi wadhamini au mashemasi wakutanike pamoja, na acha...wakutanike pamoja, na watoe uamuzi huu, ndipo wamwambie mchungaji ili ifanywe *hivi*. Basi...Basi mchungaji na aseme kuwa “Mtu *fulani* huyu,” ataje jina lake, “nasi hatumjui. Na maongozi yetu hapa ni ku—kuchunguza kabla ya kuwapa watu sadaka, na, hiyo ni kusema, watu wetu sisi. Lakini mtu huyu hapa, yeye asema amevunjika moyo, yeye alikuwa na jambo la ghafla, yeye ana watoto wagonjwa, yeye anajaribu kupata dawa kwa ajili ya watoto wake,” au cho chote kile, jambo la ghafla. Sasa, yeye anasimama papa hapa, ‘Je, waweza kusimama, bwana?” Ona, hebu yeye asimame. Na aseme, “Sasa ninyi watu tazameni yale...jinsi alivyo. Sasa, mlipata hayo kwenye...Kwa wale wanasikiza baada ya ibada hii mtu huyu atasimama pale mbele ya mlango wa mbele, na watu wakitoka, wanaojisikia wanataka kumchangia, mko huru, tunalitangaza tu kanisani.” Hauliidhinishi, unalitangaza tu. Ona, huko ni kumkaribisha mgeni. Ona? Mwafahamu sasa? Vema.

¹⁰⁹ Nadhani hayo yatosha kwa swali hilo.

230. Na kanda je? Sasa lina: Na kanda je? (Lina alama ya kuuliza) **Kwa sababu, wengi wanaandikiaa afisi barua na kukulaumia uliyotenda kwa zile kanda. Pia, kuhusu**

wengine kanisani wanaouza kanda, kama Bw. Maguire apaswa kulipa sehemu ya bei yake.

¹¹⁰ Vema, kanda zile ni kwa mapatano. Na kama nina. . . Sijui hasa mapatano hayo hasa yanaisha lini, lakini wadhamini, hili ni juu ya wadhamini; si mashemasi, wadhamini, si mchungaji, wadhamini. Wadhamini, mara kwa mara, wao hufanya mapatano, kama ninavyolielewa. Na kama hili—hili ni kosa, basi wadhamini wasahihishe. Hawa wadhamini wana mapatano na mtu anayenasa kanda, na kanda zile zina ruhusa ya serikali.

¹¹¹ Hamna mtu mwingine awezaye kunasa kanda isipokuwa aruhusiwe na mtu yule aliye na ruhusa ya serikali, nazo haziwezi kuuzwa isipokuwa iruhusiwe na mtu yule aliye na ruhusa ya serikali, kwa sababu hiyo ndiyo sheria, ona, aliyo nayo yule aliye na ruhusa ya serikali. Ona? Na kama ruhu-. . . yule aliye na ruhusa hiyo akitaka kumkubalia *Fulani na fulani* wanase kanda, hilo ni juu yake. Kama yeye ataka kuacha kila mtu wanase kanda, hilo ni juu yake; yeye akitaka kila mtu auze zile kanda, hilo ni juu ya mtu yule aliye na ruhusa ya serikali. Yapasa yeye awe na hati ndogo iliyoandikwa na kutiwa sahihi na yule aliye na ruhusa ya serikali, kunasa au kuuza kanda, kwa sababu basi yeye yuko huru kwa sheria; kwa sababu yeye asipofanya hivyo, mtu mwenye ruhusa ya kiserikali. . . Utajipasisha. . . Kama kuna mtu m—mkaidi aliyetaka kuzusha shida, yeye hakika angefanya hivyo. Isomeni hiyo ruhusa ya serikali. . . kwa sababu hiyo iko tu kama haki ya mtu aliyebuni kitabu, ona, jambo lile lile, hamruhusiwi kufanya hilo. Ni faini kubwa kufanya hilo.

¹¹² Kwa hivyo kama watu wananasa kanda, labda wana mapatano na Bw. Maguire aliye—aliye na. . . anayepata sehemu ya bei ya kanda zile. Na sasa. . . nami sijui kuhusu hilo, kwa sababu mimi siko hapa kutosha pamoja nanyi kujua vipi mambo haya yalivyo, na yanamhusu nani. Nakisia kuwa Bw. Maguire bado anayo, kwa sababu nje pale, mimi niko California au Arizona, niliko, nasikia wao bado wananunua kanda toka California. Ndugu Sothmann, baba mkwe wa Bw. Maguire, ambaye ni ndugu yetu humu kanisani. Nafikiri kuwa Bw. Maguire bado anayo, ile—ile ruhusa ya serikali juu ya hizo.

¹¹³ Na sasa, kumekuwa na malalamiko kila wakati kuhusu kunaswa kwa kanda. Sasa, kunapokuwa na malalamiko juu ya lo lote linalohusiana na hazina za kanisa hili, ni wajibu wa wadhamini kuona ya kwamba jambo hilo limerekebishwa. Ona? Haipaswi, kwa cho chote kile, kuweko na jambo lo lote.

Sasa mwaona hapa, lasema hapa kwa kadi hii hapa, kuwa:

Wanaandikia afisi barua wakikulaumu.

¹¹⁴ Hakika, nina barua nyingi juu ya haya, nami nataka nijue sababu gani hawapati kanda zao. Sasa mnajua maagano yenu na yule aliye na ruhusa ya serikali, nijuavyo mimi. . . Kanda zile,

si—sitaki uhusiano wo wote nazo, mimi mwenyewe, kama mtu ye yote aweza kutumia kanda zile kwa kueneza Injili, “Amina!”

115 Lakini, kwanza, Ndugu Roberson na wengineo walianza kunasa, Ndugu Beeler na wengine kadha wa kadha walianza kuzinasa; kisha hao vijana wawili, Ndugu Mercier na Ndugu Goad, walizinasa kwa miaka mingi; na, bila shaka, wakati kila mmoja wa watu hawa amezinasa, kumekuwa na malalamiko dhidi ya kila mmoja wao. Walakini, inaonekana ya kwamba tangu hapa hivi majuzi, kumekuwa na malalamiko makubwa kuhusu kutopata kanda zao. Watu wamenipigia simu kutoka kote nchini. Ndiposa tena, kanda zilizofutwa. Watakuwa wakisikiza jambo moja dakika moja, na kusikiza jambo lingine, ndiposa huwezi hata kufahamu ni nini.

116 Sasa, watu hawa wanaonunua kanda hizi sharti wapate kanda halisi. Sijali watafanyaje kuzipata, tunataka kuona wanunuzi wetu na Ndugu zetu (hao ni wanunuzi wetu na Ndugu zetu), na kadhalika, yapasa wawe na kanda “bora sana na za hali ya juu.” Sasa, ninyi wadhamini tekelezeni hilo, kuwa watu hawa wametoshaka. Kama hawajatosheka, pesa zao sharti zirudishwe mara moja.

117 Na mtu fulani alinipigia simu, akasema, wamengoja kanda kwa miezi kadha. Sasa, sijui jinsi Ndugu Maguire hushughulikia hili. Si—sijui hilo, kwa kuwa sijui lo lote kuhusu. Nami... Si kazi yangu kujua cho chote kuhusu hayo, hiyo ni kazi yake pamoja nao na wadhamini. Nami sijaribu kuingilia hayo lakini ninawaambieni tu masharti yake. Ona? Masharti ni kuwa kanda hizi, toka wakati wanapoziagiza kanda hizo, zinapaswa kutumwa baada ya siku moja au mbili, tatu au nne, tano; baada ya wao kuziagiza, yapasa zitumwe au ile ruhusa ya serikali inaweza kufutuliwa mbali wakati wo wote maagizo haya yasipotimizwa. Ona?

118 Sasa, na baada ya miezi sita au mwaka, hii inapaswa kuidhinishwa upya, mapatano haya yanapaswa kuidhinishwa tena. Yawapasa mkutane kwa tarehe *fulani* ambayo ruhusa hii ya serikali inasema yawapasa mkutane. Ndiposa inapaswa kuwa hivyo, hiyo ni kusema, watu wengine wanapaswa kuingia wakati huo, na mnahitajika kuwaarifu wengine ambao wamekuwa wakiuliza habari za kanda, kisha mfanye mapatano halafu mketi mkajadiliane.

119 Sasa, maagizo hayo yanapaswa kutekelezwa! Ona? Na yanapaswa kutekelezwa vema, kwa sababu kuna malalamiko. Walimlalamikia Leo na Gene, walimlalamikia kila mmoja, kuna malalamizi juu ya Ndugu Maguire, na watamlalamikia mtu mwingine, lakini hebu na tuchunguze malalamiko yao ni kuhusu nini.

120 Sasa, lakini kanda zinapoanza kulundikana, masanduku kadha, barua zikimiminika kwa madazan, nao...Ona...

halimwangukii mnasa kanda, lanijia mimi. Wao kila mara wananishambulia juu ya hilo. Sasa, ni wajibu wangu kama Mkristo kuona kuwa watu wanapata kile wanachonunua, nami nawatakeni ninyi wadhamini mhakikishe kuwa wanazipata. Kama itabidi walipishe zaidi, wanunue kanda bora, wanunue mtambo bora, tunataka mtu anayenasa kanda awe anayenasa vema. Hiyo ndiyo hamu yetu. Kanda lazima zifanywe sahihi! Na wanunuzi yapasa watoshelezwe, au tukomeshe kitu kile chote, tusiwe na kanda, tuache ye yote anayetaka kuzinasa azinase. Lakini kama wataziua, acha wao waone kuwa wanapata kile walichonunua, kwa sababu huo ndio Ukristo. Hivyo ni kama vile wewe. . .

¹²¹ Na wanapokuja hapa kusikiza Injili, nataka kuwapa iliyo bora nijuavyo kuwapa (ona?), na wajapo hapa nataka ninyi mhakikishe kuwa kila mtu na kila kitu kinatekelezwa. Hiyo ndiyo sababu nawaambia ninyi mashemasi, wadhamini, na wachungaji, hapa usiku huu, kuwa lazima mtekeleze hili vilivyo, kwa sababu watu wanakuja hapa kumtafuta Mungu, nasi yatupasa kufanya mambo haya katika taratibu.

¹²² Na pia kanda lazima ziwekwe mahali pao. Kama watalipisha zaidi, kama mna kanda duni wanazonasa, basi nunueni kanda nzuri. Kama itawalazimu kupandisha bei, ipandisheni, na watu wapate kile wanachouziwa.

¹²³ Sina haja hata kidogo na kupata pesa zake, hata senti moja, wala hata na Maskani hayana haja nazo; siwatakeni mfanye hivyo. Msijali hizo, se—sehemu ya bei yake. Kama wangelipa zingine, nakisia ingaliwapasa kuchukua sehemu ndogo ya pesa hizo kwa sababu zinafanyiwa hapa. Nadhani hilo ni jambo fulani ambalo yeye alimwambia Bw. Miller na wengineo kuhusu sheria, yatupasa kupata sehemu fulani ya bei yake na kadhalika. Hilo ni juu yenu nyote kushughulikia hilo. Sihusiki na haya kamwe ila yale. . . Hayo yamewekwa pamoja, ninyi nyote shughulikieni hayo. Siwezi kuyashughulikia yote, nawaambia tu jinsi yanavyopaswa kuwa na yanavyopaswa kuendelezwa. Hilo. . . Na mlifahamu, nilisema, “Yanavyopaswa kuendelezwa!” Kwa hivyo tunataka haya yaendelezwe barabara.

¹²⁴ Na kama mnapaswa kuwa na mtambo bora wa kunasia, basi nunueni mtambo bora. Kama hamna budi. . . Sasa, niliwaambia, nilisema, “Kila mku. . . mishi ni niendayo hudumani, kabla sijaondoka nitawajulisha ni mahubiri gani ninaenda kuhubiri nje kule, kitu fulani ambacho nimekwisha. . .” Nami niliwaahidi ninyi nyote, ambayo nitayanasa tena Jumapili usiku, ya kwamba “Kabla sijahubiri ujumbe mpya, ungehubiriwa katika Maskani haya kwanza, kwa sababu inaonekana kwamba wana vinasa sauti bora.” Mwakumbuka hilo? Ndipo ninapokuja hapa kuhubiri jumbe zangu ndipo niende tena nje na kumwarifu mtu wa kanda ni ibada gani. Wananiuliza, “Ni zipi? Utahubiri nini?” Nilimwambia, “Usiku *huu* nitahubiri *hivi* na vile na usiku

huu nitahubiri *hivi na vile*,” kwa hivyo wanazitayarisha kusudi wanunuzi wapate kuzipata papo hapo; wawe nazo, kanda bora kuliko zile wanalipata mkutanoni, kwa sababu zinafanyiwa papa hapa maskanini ambapo vipaza sauti ni bora. Ona?

¹²⁵ Sasa, basi naenda kwa mahubiri haya makuu ya injili, nitakayohubiri sasa kule ng’ambo na kadhalika, siwezi kuahidi hilo, mwaona, siwezi kuahidi kuwa nitahubiri ujumbe wangu wa kwanza hapa. Kwa sababu unapohubiri hapa na pale, hizo jumbe, yakupasa kuwa na kitu fulani ambacho...ki—kinavunda ndani yako, na hakina budi kuvunda kwa wale wanaosikiza. Sharti ufanye kitu kingine tofauti, mwaona, na ulete tu kama Ujumbe ulivyo *pale*. Lakini acha wao waweke mtambo hudumani, au cho chote kile, ambao utanasa kanda hizi kikamilifu.

¹²⁶ Tengenezeni kanda kamilifu, na kila kanda isikizwe na kuchunguzwa kabla haijaenda, au mkomesha kitu hicho chote; hata msikishughulikie kamwe, acha kila mtu ajinasie kanda zake mwenyewe. Ona? Lakini acha ifanywe vema, ona, ili manung’uniko haya yakome. Hatutaki manung’uniko yo yote. Kama kuna mung’uniko, na tuyasuluhishe, ndipo tutayakomesha.

¹²⁷ Sasa, nitaharakisha upesi niwezavyo. Billy ana maswali mawili zaidi hapa, au matatu, ndipo tutamalizia.

231. Umbali gani, Ndugu Branham, shemasi awezao au apaswao kuenda kuweka taratibu kanisani? Je, yatupasa tuweke taratibu au tungoje hata Ndugu Neville atwambie kile tunachopaswa kufanya?

¹²⁸ Hiyo si kazi ya Ndugu Neville, hiyo ni kazi yenu. Ona? Hamumwambii Ndugu Neville ahubiri nini, namna ya kuhubiri. Ona, hiyo ni kazi yenu, ninyi mashemasi, inawapasa kufanya hayo. Ninyi shughulikieni hayo. Hayo si kitu kwa Ndugu Neville, hiyo ni kazi yenu. Ona?

¹²⁹ Sasa, kama askari nje hapa barabarani akimwona mtu fulani anaiba mali nje kule nyuma ya motokaa, je, yapasa yeye amwite meya na kumwambia, “Sasa Meya, mheshimiwa, bwana, nakutumikia wewe hapa katika hiki kikosi cha polisi. Naam, nalimwona mtu fulani kule barabarani, yeye alikuwa akiiba magurudumu toka kwenye motokaa usiku uliopita. Sasa, nashangaa, wasemaje juu ya haya?” Jamani! Ona? Ona, hilo halingekuwa la busara. Sivyoy? La, bwana. Kama yeye alikuwa akitenda tendo baya, mshike.

¹³⁰ Na kama mtu anafanya kosa fulani humu kanisani, au mtu yeyote, wakomeshe, ongea nao. Usijivune; lakini kama hawatasikia, nena kwa njia ambayo watajua yale unayosema. Ona? Ona, kama ukimwambia mtoto, sema, “Rudi kule nyuma,” naye hana adabu. Mashemasi, kaeni mahali penu! Wekeni... Iwapo mko wanne, kaeni wawili mbele na wawili nyuma, kwenye

pembe hizi au mahali kama hapo. Na tazameni kwa makini mno, kwa ajili ya watu wakaidi na cho chote kile kikiingia hivi, mwaona. Na ninyi mwe macho, nanyi mwe mahali penu pa huduma na mkae pale, hayo ndiyo makao yenu; au simameni kando ya kuta na kumwalia kila mtu anayeingia.

¹³¹ Shemasi hushughulikia nyumba ya Mungu. Mtu akiingia, nena nao; mwe pale kuwasalimu, wasalimieni kwa mkono. Hiyo ni kusema, wewe ni askari, “Je, twaweza kukuonyesha chumba cha kuweka nguo?” Au “Keti, tafadhali.” “Twaweza kukupa kitabu cha nyimbo au kitu fulani?” au “Tungetaka wewe ujistareheshe mwenyewe hapa, na—na uombe, na—nasi tuna furaha wewe uko hapa pamoja nasi usiku huu.” Waongoze moja kwa moja hadi mahali fulani, na uwaulize, “Ungetaka kuwa karibu au ungetaka kuwa nyuma hapa?” au cho chote kile. Huo ni ukarimu.

¹³² Askari (au shemasi) ni polisi wa majeshi kwa jeshi, mkarimu, bali yuna mamlaka. Ona? Mwajua jinsi polisi wa majeshi alivyo, alivyo hasa, akitekeleza haki zake, nadhani yeye yuko tu kama kasisi wa jeshi. Mwaona? Ni kuheshimiana na kadhalika, lakini yeye yuna mamlaka. Ona, yakupasa umsikize. Ona, yeye aweka. . .Hawa walaghai wanaoenda nje kule wakalewa, naam, yeye huwaweka mahali pao. Vivyo hivyo naye shemasi huwaweka mahali pao.

¹³³ Sasa, kumbuka, shemasi ni askari, na afisi ya shemasi hakika ni kali kuliko karibu afisi yo yote kanisani. Sijui afisi iliyo kali kuliko afisi ya shemasi. Naam, kwa sababu yeye ana—yeye ana kazi ngumu sana, naye ni mtu wa Mungu. Yeye ni mtu wa Mungu kama tu vile mchungaji alivyo mtu wa Mungu. Bila shaka, naam. Yeye ni mtumishi wa Mungu.

¹³⁴ Sasa wadhamini, jambo ni kwamba, wako na wajibu kwa Mungu kuchunguza hazina na kushughulikia hayo, mambo yanayoendelea hivyo. Niliwaambia kuhusu kanda hizo, na—na kuhusu mambo mengine hapa yanayoendelea, kuhusu ujenzi na urekebishaji, na kukusanya pesa na mengineyo, hayo—hayo ndiyo wanayoshughulikia: mali, hazina na mengineyo. Mashemasi hawahusiki katika hayo kamwe. Wala m—mdhamini hana uhusiano na afisi ya shemasi.

¹³⁵ Sasa, kama mashemasi wanataka kuomba wadhamini msaada kwa lo lote, au—au wadhamini wawaombe mashemasi, nanyi nyote mnafanya kazi pamoja. . .Lakini huo wajibu wenu, ni kuitenganisha. Ona? Vema.

¹³⁶ Sasa, la, msimwulize Ndugu Neville. Kama Ndugu Neville akiwauliza mfanye jambo fulani, ndipo huyo—huyo ndiye mchungaji wenu, kwa kuheshimiana na upendo na kila kitu. . . Kama yeye angesema, “Ndugu Collins, Ndugu Hickerson, Ndugu Tony, au mtu fulani, waweza kutazama kuna nini pembeni

mle.” Akiwa kazini mwake hivyo, mwajua, kama mtu halisi wa Mungu.

¹³⁷ Kumbukeni, hamko kutumikia Maskani ya Branham, wala hamumtumikii Ndugu Neville au mimi, mnamtumikia Yesu Kristo. Ona? Ninyi . . . Huyo ndiye mnayemtumikia . . . Na Yeye—Yeye anauheshimu uaminifu wenu vivyo hivyo kama Yeye anavyofanya kwa mchungaji huyo au mtu ye yote yule. Yeye anatarajia uaminifu wenu! Nasi tunataka kuonyesha uaminifu wetu.

¹³⁸ Sasa, wakati mwingine huwa vigumu. Ni vigumu kwangu kule nje. Mhudumu anayeketi pale ninayempenda kwa moyo wangu wote yanipasa kumkemea sana: ona, lakini kwa upendo, nimeunyosha mkono kumsaidia. Mwaona? Nao wananijia na kusema, “Ndugu Branham, wewe ni mtu wa ajabu, mbona tusipatane kidogo kwa huo ubatizo, na kwa *hili*, *hilo*, na *linginelo*, usalama huo, na uzao wa nyoka?”

¹³⁹ Ninasema, “Ndugu, nakupenda, lakini sasa hebu tuchukue . . . hebu tuchukue Maandiko tuone nani aliye sahihi, au aliyekosea. Ona, sina budi ku . . .”

¹⁴⁰ “Ee, La. Sasa, Ndugu Branham, nakwambia, umekosea kabisa.” Ona, ananikasirikia.

¹⁴¹ “Ee,” nasema, “Vema, labda nimekosea. Basi, kama nimekosea, hakika ungeniambia, una- . . . Wajua ambapo nimekosea, basi nionyeshe nilikokosea. Nami niko tayari kusahihishwa, ona.”

¹⁴² Jambo lile lile, “Hee, haikupasi kumwambia mtoto huyo aketi.” Sasa, shemasi ni—ni mlinzi katika nyumba ya Mungu. Ona? Sasa uki- . . . Yeye hulinda nyumba ya Mungu na kuiweka katika taratibu. Sasa, hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo, na kama una cho chote kinachompasa shemasi kutenda, njoo uniambie. Ona, ni jambo lile lile. Lakini huo—huo ni wajibu wako kufanya hivyo, naam, liunge mkono tu.

¹⁴³ Na haiwapasi kumwuliza mtu ye yote, huo—huo ni wajibu wenu. Ndugu Neville hamwulizi ye yote, kanisa halipaswi kumwuliza . . . nakusudia, wa—wa—wadhamini hawapaswi waende wamwulize Ndugu Neville kama—kama yeye ataka paa iwekke juu ya maskani. Ona? La, hashu, hilo ni juu yenu. Mashemasi hawapaswi . . .

¹⁴⁴ Vivyo hivyo mchungaji naye, “Utahubiri nini? Sitaki ufanye *hili*.” Hawapaswi kusema hayo, yeye yu chini ya Mungu, ona, mchungaji wao. Ndiposa i—iwapo . . . Ndugu Neville, yeye huhubiri ujumbe ambao Bwana ametupea sisi, nasi sote tunakubaliana naye. Na nikimwambia Ndugu Neville kitu fulani kibaya, Mungu atanihukumia hicho. Naam. Ona? Kwa hivyo Mungu ndiye mkuu wa yote. Ona? Nasi tunafanya tu kazi kama mabalozi Wake, mwaona, chini hapa katika afisi hizi.

232. Tafadhali...(Swali linalofuata, ndiposa nadhani tuna moja zaidi kisha tuta—tutakoma.) **Tafadhali eleza kanisa jinsi karama za lugha zitakavyofanya kazi katika kanisa letu. Nimefanya hivyo. Kanisa laweza kuwekwa katika taratibu lini kama...au ambapo karama inafanya kazi? Tumekwisha eleza hilo.**

233. Ni k-r-i-s-m-a-s-i ngapi...waweza kuona hilo ni nini? [Billy Paul amjibu Ndugu Branham, “vinanda”—Mh.] Ee, vifaa. **Ni vinanda vingapi ambavyo yatupasa kuwa navyo kanisani mbali na kinanda cha mabomba na piano?”**

¹⁴⁵ Vema, yategemea kama mlikuwa na bendi ya zeze au cho chote mlichokuwa nacho, mwaona. Sijui mlichu nacho, sifahamu maana ya hili. Lakini kile kinanda cha bomba na piano ni mali ya kanisa. Sasa, kama mwongoza nyimbo angependa kuwa na tarumbeta na parapanda na vinginevyo kama hivyo, na mtu fulani huja kanisani nao hupiga vinanda hivi... Nao wako katika kundi la waimbaji, ha—hatimaye, bila shaka, basi hilo ni juu ya wadhamini wenu, kushauriana na wadhamini na kuona kama wana pesa za kununulia vinanda na kadhalika, au vyo vyote hivyo. Nadhani hilo ndilo swali lao.

¹⁴⁶ Lakini kama wana vinanda vyao wenyewe, ni vizuri sana. Kama hawana, nao ni washiriki hapa wa kundi la waimbaji, si mtu anayepitia hapa na kupiga mara kwa mara, na kuondoka hivyo, yapasa liwe kundi la waimbaji kanisani. Kanisa halitamnunulia ta—ta—tarumbeta mtu anayeipigia hapa na kesho usiku mahali pengine, na mahali pengine, na aingie mara kwa mara na aipige kidogo. La, bwana. Yapasa liwe kundi la wapiga vinanda wa mumu humu, kundi halisi la waimbaji lililo na ki—kiongozi, ndiposa kanisa, ongeeni nao kuhusu kununua vinanda.

234. Tafadhali eleza jinsi itupasavyo ku-...jinsi sisi mashemasi tunaweza kuwatuliza watu madhabahuni kabla au baada...Tafadhali eleza. [Billy Paul amsomea Ndugu Branham swali, “Tunawanyamazishaje watu madhabahuni kabla na baada ya kanisa?”—Mh.] Ee, vema.

¹⁴⁷ Ningeshauri hivi, ndugu. Sasa, hilo ni jambo mhimu sana, laiti tungelikuwa na wakati zaidi wa kulijadili maana ni—ni... li—linamaanisha jambo fulani kwetu, ona. Sasa, kanisa si...

¹⁴⁸ Kama yeye ataka ku...Kama mnataka kusikiza kanda hii usiku fulani na kuicheza mbele ya mikutano, ili watu wayafahamu basi ichezwe; sehemu hii tu ya kanda kama si zaidi, hii tu. Sehemu yo yote ya hii mnayotaka isikizwe kwa ajili ya jambo fulani, endeleeni tu kuicheza hadi muipate, kisha mkaicheze. Ona, kwa sababu ni maswali.

¹⁴⁹ Sasa, mashemasi wa kanisa, na kama ni—kama nilivyosema, ni askari wa kanisa. Lakini kanisa si nyumba ya mikutano yote kwa ajili ya—kwa ajili ushirika na urafiki na michezo. Kanisa

ni madhabahu ya Mungu! Tunakuja hapa...Sasa, tukitaka kukutana wenyewe kwa wenyewe, hebu niye nyumbani kwako au uje nyumbani kwangu, au tembeleaneni manyumbani ninyi kwa ninyi mkakutanike. Lakini kuchezea humu kanisani, na kuzungumza na mambo kama hayo, si haki, ndugu zanguni; tunakuja hapa, tunaondoa mambo yote mawazoni mwetu. Kama tungekuja hapa...

¹⁵⁰ Tazama jinsi tulivyokuwa tukilifanya miaka mingi iliyopita. Dada Gertie alikuwa mpiga kinanda. Nilipokuwa mchungaji hapa, ili—ilininipasa kuwa mchungaji, shemasi, mdhamini na kila kitu wakati mmoja, ona, lakini ili—ilininipasa kufanya hivyo. Sasa haiwapasi kufanya hivyo, ona, kwa sababu mna watu wa kutekeleza hayo. Lakini wakati... Nilikuwa na mabawabu, Ndugu Seward na wengine wote mlangoni. Walikuwa na vitabu vimerundikana pale mlangoni, wameketi kitini, au cho chote kile. Na mtu ye yote alipoingia, mliwaonyesha mahali pa kutundika makoti yao, au kuwaongoza kwenye viti vyao, kuwapa kitabu cha nyimbo na kuwauliza “waendele kuomba.” Basi kila mtu aliketi kitini mwake na kuomba kimya hadi wakati wa kuanza. Ona? Ndiposa wakati wa kuanza, Dada Gertie, mpiga kinanda, alikuja pale na kuanza kucheza mziki kabla... wakati watu wana—wanapokusanyika.

¹⁵¹ Ningeshauri mpiga kinanda wenu aende pale na mziki mzuri sana. Na kama hawezi kuwa hapa, chezeni kanda, au cho chote kile. Na mwe na muziki, wimbo mzuri na mtakatifu ukiendelea. Kwa hivyo... Kisha mwaulize watu... Na kama watu wakiendelea kuongea na kufanya yasiyofaa, acha mmoja wa mashemasi aende kwenye kipaza sauti pale dawatinini aseme, “Shii, shii, shii,” hivyo. Aseme, “Hapa maskanini, tuna—tunawataka mje mkaabudu. Na tusifanye kelele sana, sikizeni muziki. Chukua kiti chako, keti, kuwa mtulivu (ona?), omba au soma Biblia. Hapa madhabahuni ndipo Bwana aishipo. Nasi tunataka kila mtu awe mtulivu na aabudu, si kukimbia hapa na pale, kuongea kabla ya ibada. Kutaniken wenyewe, nanyi mmekuja hapa kuongea na Bwana. Ona? Au uendele kuomba kimoyomoyo, ona, au usome Biblia yako.”

¹⁵² Nilipoingia katika kanisa liitwalo Marble kule kwa—kwa... Norman Vincent Peale, mumemsikia, mwaona. Nami niliingia katika... Mwanasaikolijia mashuhuri, yeye ni mwalimu, mwajua. Nami nilienda katika kanisa lake, niliwaza tu kuwa, “Laiti maskini yangu yangelifanya hayo tena.” Hao mashemasi wamesimama papo hapo mlangoni unapoingia. Wao, bila shaka, wanakupi kijikaratasi cha shule ya Jumapili, wanakuingiza moja kwa moja ndani. Iliwapasa kuondoka mara tatu, mwajua, linachukua tu yapata watu mia nne au tano, mwajua; na New York ni mahali pakubwa, naye ni mtu mashuhuri. Nami nafikiri iliwapasa kufanya darasa moja saa nne asubuhi na nyingine saa tano, mahubiri yale yale yakirudiwa tena, ibada ile ile

hasa, karatasi ile ile. Lakini walipoondoka, nao walikuwa na (naamini) dakika tano kwa kanisa kuwa tayari... Hakuna mtu mwingine angeingia hadi wametoka nje, ndipo mashemasi walifungua njia na kanisa lingine lilijaa. Walikuwa na vile viti vya masanduku vya kale, mwajua wanaingia ndani *hivyo*, na kuketi katika marefu ya kanisa ambapo mnafungua mlango. Na ni mtindo wa kale, limedumu pale kwa—kwa karibu miaka mia mbili, nakisia, lile kanisa la kale la Marble.

¹⁵³ Nawe ungesikia sindano ikianguka po pote katika kanisa hilo, na kila mtu katika maombi kwa muda usiopungua dakika thelathini kabla wimbo wa kwanza haujaimbwa na kinanda, unaotangulia. Na kila mtu ako katika kuomba. Niliwaza, “Ni ajabu jinsi gani!” Ndipo wakati mhudumu huyo... Hayo matangulizi, yapata... nadhani walipiga mmoja wa kutangulia dakika tatu hadi tano, *Jinsi Wewe Ulivyo Mkuu*, au kitu kama hicho, na kuendelea hivyo. Na walipofanya hivyo, kila mtu aliacha kuomba na alikuwa akisikiza matangulizi yale. Ona, inabadilisha, toka kwa maombi hadi kwa matangulizi. Basi walipopiga huo, ndipo yule kiongozi wa kwaya alisimamia kwaya. Kisha wakaimba wimbo wa makutano *pamoja na* pambio. Ndiposa wakajitayarisha kwa darasa lao la shule ya Jumapili. Ona? Basi basi yalipokwisha, hakuwa na kitu kilichoendelea isipokuwa kuabudu kwa kiungu, kila mara, hilo ndilo linalotuleta hapa.

¹⁵⁴ Nami nadhani lingekuwa jambo nzuri kama kanisa letu... Nami nasema tu hili, tutafanya hivyo. Ona? Na tulitekeleze. Mtu fulani akifanya lo lote, jambo lile... Nadhani lingekuwa jambo nzuri. Kama ni jambo nzuri, basi na tulifanye. Ona? Hatutaki kutupilia mbali kitu cho chote kizuri, tutafanya hivyo, haidhuru. Ona? Na kuendelea na—na kusimama juu pale na kama wakianza asubuhi, au kitu kama hicho, watu wana kazi nyingi, acha tu mtu mmoja, au mmoja wa—mmoja wa mashemasi, au mtu ye yote yule aende pale na kusema, “Imeamrishwa katika Maskani haya hapa...”

¹⁵⁵ Sijui kama wao wanafanya hivyo, wao huenda—wao huenda wanafanya hivyo. Siwi hapa daima, mwaona, sijui. Siwi hapa kabla ya ibada.

¹⁵⁶ Na wanapoingia nao wanaanza kuongea, hebu mtu mmoja aende juu pale na akaseme, “Shii—shii—shii, hebuni kidogo.” Ona? Hebu—hebu... mlete maskini yule Dada, mlete pale mkamwambie achezze muziki. Msipofanya hivyo, zinaseni kwenye kanda na ziacheni pale, ona, nyimbo za kinanda. Na msemi, “Sasa tuta... Kuna kanuni mpya Maskanini. Watu wanapoingia humu, haitupasi kunong’onezana wala kuongea, lakini kuabudu. Ona? Sasa, katika dakika chache tu ibada itaanza. Hadi wakati huo, soma Biblia au uinamishe kichwa chako uombe kimoyomoyo.” Na wakati mchache kama huo, wote watajifunza. Ona? Ona?

¹⁵⁷ Mnasikia mtu fulani akiongea, ndiposa inafikia...maana baada ya wakati mchache hivyo, baada ya muda mchache mnafikia mahali ambapo mtu fulani asema...Unaona mtu fulani akinena, hakuna mwingine ananena, mwoana, vema, ndipo mmoja wa mashemasi aje humu na kusema, "Tuna—tunawataka muabudu wakati wa ibada, mwaona?" Ona? Ona, si nyumba ya maongo, ni nyumba ya kuabudia. Mwafahamu?

Nadhani ilikuwa hivyo: **Tafadhali eleza...**(Naam. Hebu tuone. Naam)...**Tafadhali eleza jinsi ya ku...ipasavyo mashemasi...madhabahuni.** Naam, hivyo tu. Naam.

Vema, sasa hili ndilo la mwisho:

235. Ndugu Branham, tunapokuwa na nafasi mwanzoni mwa ibada nina—nina...malala-...La, walikuwana "malalamiko." Imeandikwa kwa mwandiko mdogo sana. **"Na nimekuwa na malalamiko,"** sivyo? [Billy Paul ajibu, "Enhee," na aendelea kumsaidia Ndugu Branham kusoma, hayo Maandishi madogo—Mh.]...**nilikuwa na malalamiko mwanzoni mwa ibada. Tuna...**(hebu tuone)...**Tuna—tuna—tuna nyimbo, ushuhuda, na maombi, na haja za wanaohitaji maombi, nyimbo maalum, na 1-a-b-...labda kuingilia...kuingilia ujumbe saa tano, ku...au baadaye, lakini hatuna wakati mwingi sana kwa ajili ya Neno. Watu wengine huchoka hata ikawalazimu kuondoka kabla ha—ha-...kabla—kabla haujakwisha. Ni...Tafadhali eleza ni nyimbo ngapi, na wakati upi wa kuanza ujumbe. Na wakati—wakati mwingine tunakuwa na haja ya wanaohitaji maombi—maombi na inaishia kwa mkutano wa ushuhuda, mambo fulani ambayo—ambayo haya... hayaonekani yanafaa wakati huo.**

¹⁵⁸ Sasa, natumai nimepata hilo. Billy anajaribu kunisaidia hapa. Walio kwenye kanda, mnapaswa...mtu fulani kati yetu huenda...mkutanoni, katika ibada, akisikiza jinsi haya yalivyokuwa, ni Billy akijaribu kunisaidia kulisoma kwa sababu limeandikwa kwa mwandiko mdogo sana, nami singeusoma. Nimepata fununu yake, ni kwamba, "Yatupasa tuimbe nyimbo ngapi kabla hatujaanza ibada, na ibada yapasa kuanza saa ngapi?"

¹⁵⁹ Sasa, jambo la kwanza ninalotaka kufanya hapa ni kuungama. Na ninapokosea, nataka kukubali "Nimekosea." Ona? Nami—nami ninataka kuungama hapa kwamba "Yaonekana kama kwamba mimi ndimi kiongozi wa hilo." Kwa sababu ni mimi ni—ninayefanya hizi ibada ndefu na kadhalika, ndiyo yaliyoliweka kanisa katika mtindo huu (ona?) wa kufanya hivyo, lakini haipasi kuwa vile. Na sasa, kumbukeni, nime... nina...Nilikuwa nawaambia ninyi nyote, "Jumapili usiku, Bwana akipenda, Jumapili usiku, kwamba, najaribu kupanga ibada zangu tangu sasa, kama itanilazimu nikae juma moja

zaidi, ziwe za dakika thelathini au arobaini kwa ibada yangu ndefu sana.”

¹⁶⁰ Kwa sababu nimeona hili, kuwa ibada ambayo...Ni muhimu sana, na ujumbe unatolewa katika nguvu; ukiendelea sana, inawachosha watu nao hawafahamu. Sababu ambayo nimekuwa nikitoa...Nilijua hilo wakati wote. Ona? Wanenaji waliofanikiwa sana ni wale walio na...Yesu alikuwa mtu wa maneno machache, chunguza mahubiri Yake. Chunguza mahubiriya Paulo siku ya Pentekoste, labda yalimchukua yeye dakika kumi na tano, naye aliingiza...pale, kitu fulani amba—ambacho kiliwaingiza watu elfu tatu katika Ufalme wa Mungu. Ona, moja kwa moja hadi kwa lengo. Ona?

¹⁶¹ Nami—nami nina hatia. Kwa sababu, sababu ya kufanya hili, si kwa sababu sikujua, lakini ninanasa kanda (ona?), na kanda hizi zitasikizwa manyumbani kwa masaa kadha wa kadha. Lakini kama mtakavyogundua Jumapili ijayo, sababu ya kutenda hayo, hii Jumapili inayokuja, sababu nimefanya mambo haya...Huenda nikasema sasa hivi kwenye kanda. Mambo haya nimeyafanya kwa sababu ya mzigo mkubwa mno ulio juu yangu kuhusu Ujumbe wa wakati huu, kuusambasa. Sasa Ujumbe umetolewa, sasa mimi huchukua dakika thelathini au kitu kama hicho, tangu mwanzo wa mwaka huu, katika mikutano yangu kule nje...kila mahali niendapo, na kujaribu na hata kuweka saa yangu kwa dakika thelathini, au si zaidi ya arobaini zikiwa nyingi sana: nikaumaliza Ujumbe huo, na kutoa wito wa madhabahuni kama nina-...au lo lote niendalo kufanya, ama kuagiza mstari wa maombi; na nisichukue wakati huo mwingi, kwa sababu unawachosha watu. Najua hilo.

¹⁶² Lakini tazama hapa. Nakisia, mwaka huu, hatujakuwa na watu dazan waliosimama na kuondoka, na wakati mwingine nawakawisha hapa kwa masaa mawili na matatu. Ona? Naam. Kwa sababu imekuwa kunasa kanda hizi zinazoenda ulimwenguni kote (ona?), na watu nje kule, wataketi kwa masaa kadhaa na kusikiza Huo; na wahudumu, na kadhalika, Ujerumani, Uswiss, Afrika, Asia, na kila mahali, ona, wakisikiza Hizo.

¹⁶³ Lakini, ona, kwa ajili ya madhabahu, kwa ajili ya kanisa...Na hilo ni Sawa. Kama uko hapa ukinasa kanda, na una kanda ya masaa mawili, weka ujumbe wa masaa mawili kwake; lakini kama hauko kunasa kanda kwa kitu kama hicho, basi fupisha ujumbe, ona, fupisha ujumbe. Nitawaambia sababu yake, kunao wengine wanaojazwa upesi, na wengine hukaa sana, ona, hivyo, na yakupasa uwe na wastani wa kuwaridhisha hao.

¹⁶⁴ Na sasa, wakati mwingi ambapo tunaharibu ibada zetu kwa mkutano uliocholewa sana wa ushuhuda, nami najua nina hatia ya kufanya hayo. Na mliondoka nje tulipokuwa na mikutano barabarani, na kuacha ndugu mzee asimame nje

pale, naye atasimama kule nje. . . Kisha mkimuuliza aombe, basi atamwombea mkuu wa mji, na mkuu wa jimbo, na wa Rais wa nchi, na—na kila mtu hivyo, na wachungaji wote pale, mwajua, kila mmoja kwa hesabu, na Dada Amina aliye hospitalini, na mambo kama hayo; huku watu wamesimama, wanapita—pita kwenye mkutano wa barabarani wanaendelea—wanaendelea tu kupita-pita. Ona? Yeye anawachosha. Vema, ku- . . .

¹⁶⁵ Ona, jambo muhimu sasa, ombi lako lapaswa kuwa katika siri, ombi lako muhimu, lile refu. Omba yote. . . Ingia katika chumba cha faraghani, funga mlango. Humo ndimo unamopaswa kuomba siku nzima, usiku wote, au masaa mawili, ombea mle. Lakini ndani humu, wakati unaposikizwa na watu, fanya maombi yako yawe mafupi, maombi ya haraka. Fanyeni ibada zenu zote. . . Na wekeni mwingi sana wa ibada yenu kwa Neno. Hilo ndilo jambo muhimu! Ingiza Neno hilo kwa nguvu uwezavyo. Ona, wape watu Neno.

¹⁶⁶ Naam, shauri langu ndilo hili. Sasa, kumbukeni basi, nimeungama kuwa nina hatia ya kuanzisha haya. Lakini basi nimewaambia sababu ya kuanzisha haya, ninanasa kanda za masaa mawili kuzituma nchi za ng'ambo na kila mahali, za Ujumbe, mwaona. Lakini kanisa halipaswi kufuata hayo (ujumbe hapa Maskanini) baada ya kanda hizo (masaa mawili) kupelekwa mahali mbalimbali, ona, na kutoka nje hivyo.

¹⁶⁷ Sasa, hii ndiyo taratibu yenu. . . Hebu niwapeni mfano, Je, hilo ni sawa, shauri? Ningesema kuwa kanisa lapaswa kufungua milango yake wazi saa fulani, waumini waingie, huku nyimbo zinapigwa. Na kila mtu aingie akaabudu, si kutembeleana. Na usiwaambie watembeleane baadaye, waambie “ondokeni mwende zenu, si kutembeleana. Kama ulitaka kutembeleana, kuna nafasi kubwa kule nje. Lakini haya ni madhabahu, na pawekwe pasafi.” Sasa, kama Roho wa Bwana anatenda kazi hapa, na tupawekee Roho wa Bwana. Ona? Na—na atazidi kutenda kazi. Msipofanya hayo, sikizeni maneno yangu, litaanguka; hakika litaanguka. Na hebu tuyaweke, ni wajibu wetu, hiyo ndiyo sababu mimi niko hapa usiku wa leo. Na tuweke mambo haya katika taratibu pamoja na hizi—na taratibu hizi.

¹⁶⁸ Sasa tazama, ningesema hili. Kwa kawaida, isipokuwa tumetangaza waziwazi. . . na kuwaambia utanasu ujumbe. Ona? Sasa, kama Nduku Neville ana ujumbe hapa ambao yeye anaenda. . . yeye anaenda. . . yeye ana ujumbe ambao anataka kuwapelekea watu, kwa kanda, au cho chote kile, aseme, “Sasa, Jumapili ijayo usiku tutanasu kanda ya masaa mawili,” kanda ya masaa matatu, au cho—cho chote kile. “Tutatoa kanda ya masaa mawili au matatu,” cho chote kile, “Jumapili ijayo usiku.” Ndiposa watu watajua. Kisha wanapoingia, useme, “Sasa, tutanasu ujumbe usiku huu. Nami nina ujumbe hapa ambao ni mojawapo wa. . . nataka unaswe na kusambaswa. Nimekuwa. . . nasikia nikiongozwa kusambaswa ujumbe huu. Na utanaswa,

huenda ukachukua masaa mawili,” masaa matatu, au yo yote yale, useme hivyo.

¹⁶⁹ Lakini, kwa kawaida, kama tu nifanyavyo ninapoenda mahali kama mojawapo wa mikutano ya Wafanyi Biashara Wakristo, au niko nje katika mikutano yangu nje kule kwa mastari wa wanaohitaji maombi, kama ningalisimama kule na kutoa ujumbe wa masaa matatu usiku mmoja kabla ya ibada ya uponyaji, mwaona linaponiweka mimi? Ona? Naam, watu, usiku unaofuata waumini wako ni nusu ya waliokuweko. Ona? Kwa sababu hawawezi kuustahimili, inawabidi waende kazini na kadhalika.

¹⁷⁰ Ningeshuri hivi, ya kwamba kwa kawaida...Sasa, nilimtaazama Ndugu Neville usiku uliopita alipohubiri. Sasa, najua sisi sote...Huo ulikuwa ujumbe wa kusisimua. Nilivandika kwa muhtasari, ninao mfukoni mwangu, naweza kuutumia kwa ujumbe mwingine wangu. Naam. *Njia ya Kuepukia*, ona, na huo ulikuwa ujumbe wa ajabu. Mwaona jinsi alivyomaliza huo mapema? Ona, yapata dakika thelathini na tano, ona, naye—naye aliumaliza. Ona? Sasa, hilo lilikuwa jema. Sasa, na Ndugu Neville, kwa desturi jumbe zake ziko hivyo. Ona, hizo si ndefu. Ona? Lakini mahali mnapoiharibia mikutano yenu ni hayo mambo yanayoitangulia. Ona?

¹⁷¹ Sasa, na—na mnapofanya hivyo...Sasa, najua, na sasa tazama, sisemi hayo kwa kutowaheshimu ninyi wadhamini, au mashemasi, au—au mchungaji, lakini nawaambieni tu: muone yaliyo Kweli, na hivi ndivyo ipaswavyo kuwa. Sasa, ninyi... kinachosababisha hayo, sasa, kila mtu, ninyi nyote mna hisani, kila mmoja wenu watu ana hisani. Kama haingalikuwa hivyo, ningesema, “Wote ila Ndugu *Lulani*, yeye hana hisani, sisi sote tunamwombea.” Lakini ninyi—ninyi mna malezi mema, nanyi mu wavumilivu, wapole, watu wapole. Hilo ni zuri, lakini msiwe walegevu kwa hayo.

¹⁷² Yesu alikuwa mtu mwenye hisani, pia, lakini ulipofikia wakati wa kusema mambo, “Imeandikwa, ‘Nyumba ya Baba Yangu ni nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya pango la wanyang’anyi.’” Ona? Yeye—Yeye alijua wakati wa kunena na wa kunyamaza. Hilo—hilo—hilo ndilo litupasalo kufanya. Ona? Hajatokea—hajatokea mtu kama Yesu, Yeye alikuwa Mungu. Na kumbuka, Yeye hata...Nena kuhusu kuwa shemasi kanisani, Yeye—Yeye alitwaa mamlaka! Alifanya kikoto cha kamba, naye hakuwaondoa nje kiungwana, aliwapiga akawafukuza nje (ona?), katika kwa nyumba ya Mungu. Naye alikuwa akifanya kazi ya shemasi kama mfano kwenu mashemasi. Ona, Yeye alikuwa mfano wenu. “Na sasa, ime—imeandikwa, ‘nyumba ya Baba Yangu ni nyumba ya Sala.’” Sasa, kumbukeni, Yesu alikuwa shemasi pale, nanyi mwajua Yesu alikuwa anafanya kazi ya shemasi.

173 Alipofikia sehemu ya mchungaji, alisemaje? “Ninyi Mafarisayo vipofu, viongozi wa vipofu!” Ona, Yeye alikuwa akichukua sehemu ya mchungaji wakati huo.

174 Naye alipowaambia yale yatakayotendeka, Yeye alikuwa amechukua kazi ya nabii. Ona?

175 Nao walipoagiza kodi ilipwe, Yeye alichukua sehemu ya mdhamini, “Petro, kwenda kule ukatupe ndoana mtoni, na samaki wa kwanza utakayemvua ana pesa mdomoni mwake. Zilipe, ona, lipa madeni yako unayodaiwa kwa haki.” Kasema, pia, “Vya Kaisari mpeni kaisari, na vya Mungu mpeni Mungu.”

176 Yeye alikuwa mchungaji, nabii, mdhamini, na shemasi. Ndivyo hakika! Kwa hivyo basi mwaona yale Yeye alifanya, na hayo yawe mfano kwenu humu nyumbani katika haya Maskani ya Branham, kwa kuwa tunataka kuwa nyumba ambayo Yeye ataheshimiwa kwa kila kitu, kila afisi, kila mahali, kusudi kusiwe na upungufu. Kuwe na upole, na uzuri, na wema, kila kitu kiwe laini kabisa, kila mtu katika wajibu wake. Ona? Hiyo ndiyo, hivyo ndivyo anavyotaka. Yeye hakusitasita. Ilipofikia wakati wa kusema, kutaja *cho chote kinaganaga*, Yeye alikitaja. Ilipofika wakati wa kuonyesha upole, basi Yeye alionyesha upole. Yeye alikuwa mpole, mwema, anayefahamu; lakini mkali, na alitenda kila kitu sawa sawa kabisa, naye alifanya hayo kama mfano kwenu. Sasa, Roho Mtakatifu alinipa tu hilo. Kwa hivyo sikuwahi kuwazia hilo, Yeye akiwa shemasi, hapo mbeleni, bali alikuwa vile. Ona? Yeye—Yeye alitenda kama shemasi.

177 Sasa nasema hili, tuseme kama ibada zenu zinaanza saa moja na nusu, kama ni wakati huo, fungueni kanisa lenu nusu saa mapema, saa moja. Hebu mpiga piano... Mwambie mpiga kinanda... Je, mnamlipa? Je, mnamlipa mpiga kinanda cha bomba? Je, analipwa, au yule mpiga piano? Yeye anafanya kwa kujitolea. Mwulizeni kwa upole. Hata kama yeye anataka alipwe, kumpa yeye kitu kwa ajili ya hilo, mwambie tunamtaka nusu saa kabla ya ibada. Na kama yeye asema, “Vema, Siwezi kufanya hivyo,” au cho chote kile, alalamike, basi mwache yeye aje hapa na anase kanda za nyimbo kadhaa nzuri za kinanda cha bomba. Mwaona? Ndiposa... weka hizo kwenye... Si lazima awe hapa kila wakati, chezeni kanda zenu. Ona? Acha mmoja wa mashemasi, wadhamini, au ye yote afunguaye, bawabu, aiweke iimbe pale, ile kanda iimbe, na iimbe huku watu wanaingia. Ona? Kwa sababu kama mashemasi hawako humu, au mtu fulani, hebu wadhamini au mtu fulani awe hapa akafanye hivyo ndiposa iimbe kwa nusu saa.

178 Lakini ifikapo saa moja na nusu, basi kengele iliyo juu ya jengo ipigwe. Ona? Je, kengele yenu ingali kule nje? Naam. Vema, acha yenu na ilie saa moja na nusu, na hilo maana yake ni kuwa hatutatembea huku na huku kanisani na kusalimiana na akina Juma na kadhalika. Kiongozi wa nyimbo na awe kazini!

Kama hakuna kiongozi wa nyimbo pale, basi mashemasi waone kuwa kuna . . . au . . . waone kuwa kuna mtu wa kuongoza nyimbo kengele hiyo ianzapo kulia. “Fungueni vitabu vyenu vya nyimbo, nambari *fulani*.” Na iwe saa—saa moja na nusu kamili.

¹⁷⁹ Vema, ndipo muimbe wimbo wa waumini, halafu labda wimbo wa pili wa waumini, kisha mtu fulani aliyetajwa awali (mkiweza) aongoza katika maombi. Na—na mchungaji, awaye. . . Vema, mchungaji, hapaswi kuwa pale, ki—kiongozi wa nyimbo apaswa kufanya hayo. Ni Ndugu Capps, nadhani. Ona, yeye angejua afanye nini, basi na—na amchukue mtu aliyetajwa . . . au yeye mwenyewe aongoze katika maombi. Awaambie makutano wasimame kwa maombi. Sasa, msipochunga. . .

¹⁸⁰ Sasa, tunaamini kuwa kila mtu apaswa kuja katika nyumba ya Mungu na kuomba, hapa ni—hapo ni mahali pa maombi. Lakini unapokuwa hapo madhabahuni, hifadhi wakati wako. Ona? Ukiwaita watu wote madhabahuni utaona kuwa kutakuwa na mtu fulani atakaa pale kwa dakika kumi na tano, ishirini, na wakati wenu wote umekwisha.

¹⁸¹ Na kwenu. . . ona, kuomba kwenu ni nyumbani. Yesu alisema, “Msalipo, msisimame kama wafanyavyo manafiki, na—na kwa muda mrefu. . . labda sala ndefu, na kusema *hili, hilo*, au *linginelo*, na—na yote kama hayo kwa kujionyesha.” Ona? Yeye alisema, “Usalipo. . . sai, ingia katika chumba chako cha ndani, chumba cha faraghani, funga mlango wako; sali mbele za Baba yako aonaye sirini, Yeye atakujazi.” Sasa, hivyo ndivyo unavyofanya maombi sirini, hivyo ndivyo yeye alivyosema itendwe.

¹⁸² Lakini wakati ninyi, mtu fulani, wanapoingia, kama kiongozi wa nyimbo, aseme, “Vema. . .” Baada ya wimbo wa kwanza, basi hebu mtu mmoja aombe, ye yote yule, ombi fupi tu. Usisimame na kuombea wakuu wote wa majimbo, na mambo kama hayo. Kama kuna haja zo zote za maombi, na ijulikane, na yaletwe, yaitize. Yaandike, useme, “Hapa.” “Usiku huu, katika kuomba, tunamkumbuka Dada *Fulani*, Ndugu *Fulani* katika hospitali, *Fulani*, na *Fulani*, na *Fulani* Wakumbukeni katika maombi yenu mnapoomba. Ndugu Juma, atatuongoza katika maombi. Na tusimame.” Ona? Na yawekwe jukwaani. Waambie, na wazoe hayo, “Kama mna haja ya maombi, iwekeni hapa, juu hapa.” Msiwe mkisema, “Nani ana mahitaji sasa, na ijulikane kwa. . .” Ndiposa, jambo la kwanza, mtu fulani atasimama na kusema, “Mungu atukuzwe! Basi mnajua. . .” Anaanza hivyo, na muda si muda, wakati mwingine ni nusu saa kabla hajaketi. Ona?

¹⁸³ Tunahusika kwa kanisa hili, si mengine; huu ni wajibu wetu kwa Mungu. Afisi hizi ni wajibu wenu kwa Mungu. Ona? Nia yangu ya kusimama hapa usiku huu, nikiwaambia ninyi haya

yote, ni kwa sababu ni wajibu wangu kwa Mungu; ni wajibu wenu kulitekeleza. Ona?

¹⁸⁴ Sasa, na wakati kitu fulani kama hicho...acha mtu fulani aongoze kwa maombi, na wanapofanya hivyo, hilo ni zuri, hebu waongoze katika maombi kisha waketi.

¹⁸⁵ Na kama mna—mna maombi maalum. Sasa, singesema hili, singeendelea...Na kama mtu ye yote anataka kuimba wimbo maalum, itangaze kanisani. Waambie kwamba Nyimbo zo zote maalum, au cho chote kitakachoimbwa, hebu waonane na kiongozi wa nyimbo kabla kanisa halijaanza. Na iwe...Sema, “Vema, nasikitika Ndugu, ningetaka...hakika ningetaka kufanya hivyo, bali ni—nina nyimbo maalum za kutosha usiku huu. Labda uniambie utakuwa hapa usiku fulani, nitakutia orodhani. Ona, orodha yangu ya mambo ndiyo hii hapa.”

¹⁸⁶ Ba—basi Ndugu Capps au ye yote anayeongoza nyimbo...na muwe na kiongozi wa nyimbo, ye yote yule. Na msiwaache wasimame na kusema...au waendele sana, wao ni wahubiri, ona. Hebu wasimame pale na kuongoza nyimbo, hiyo ndiyo kazi yao.

¹⁸⁷ Ni kazi ya mchungaji kuhubiri, ona, si kuongoza nyimbo. Yeye hapaswi kuongoza nyimbo, kiongozi wa nyimbo huongoza nyimbo. Yeye anahusika, na yapasa aje moja kwa moja chini ya upako wa Roho Mtakatifu, toka afisini mle, mahali fulani, ufikapo wakati. Yeye hata hapaswi kuwa jukwaani haya yanapoendelea. Basi na akae afisini mwake nyuma kule, ona, au nyuma humu, au kote kule, na maikrofoni hapa itauleta (ona?) wakati ukifika. Anaposikia huo wa mwisho...kama kunao maalum, kama wimbo wa mtu mmoja, wimbo wa watu wawili, au cho chote kile, kwa wimbo wenu wa tatu. Ona?

¹⁸⁸ Basi mmeimba nyimbo mbili za kusanyiko, maombi, sadaka zenu (kama mtazichukua). Na kila mtu awe mahali pake pa kazi. Useme, “Vema, tunapoimba huu wimbo wa mwisho sasa, kama mabawabu wata—watakuja mbele kwa ajili ya sadaka ya jioni.” Ona? Na watakapomaliza kuimba wimbo huo, ndio hawa mabawabu wamesimama hapa. Usema, “Vema, sasa tutaomba,” nao wanaomba, “Tunataka kumkumbuka *Fulani* hapa, na *Fulani*,” na kusoma hayo yote, mwajua, hivyo, hivyo. “Vema, kila mmoja asimame. Ndugu, tafadhali utuongoze katika maombi.” Ndipo yote yamekwisha.

¹⁸⁹ Ndipo hali wakiimba huu wimbo wa pili, au wo wote mnaoimba, mna-...chukueni sadaka yenu kama mtachukua sadaka. Uache...Ningechukua wimbo wenu wa kwanza, kisha mtoe sadaka zenu za jioni, kisha muendele na wimbo wenu wa pili, halafu muendele hivyo. Kisha wimbo wenu wa mwisho hapa...Na wimbo wenu wa mwisho, ona, uwe wa kumwalika mchungaji wenu. Na mara tu wimbo huo wa mwisho unapoimbwa, basi kinanda na kianze na matangulizi ye—yenu,

mchungaji wenu atoke. Ona, kila kitu ni sawa, kila mtu ni mtulivu. Hakuna lingine tena la kusemwa. Kila shemasi yuko mahali pake pa kazi. Mchungaji amesimama pale.

¹⁹⁰ Yeye aingia, asalimia kusanyiko lake, afungua kitabu chake na kusema, “Usiku huu, tutasoma toka kwa Biblia.” Ona, baada ya kupapata, “Tunasoma toka kwa Biblia.” Na ni jambo zuri wakati mwingine ukisema, “Katika kuliheshimu Neno la Mungu, na tusimame kwa miguu yetu tunaposoma neno.” Ona, ndipo usome, “Usiku huu ninasoma toka Kitabu cha Zaburi,” au po pote. Au acha mtu mwingine aisome, yule kiongozi wa nyimbo, au msaidizi, mtu fulani pale aliye pamoja nawe; na ayasome, yo yote yale; lakini ni heri ukiyasoma mwenyewe, ukiweza. Ndipo isome hivyo, halafu chukua somo lako. Ona? Na wakati kama huo, mmetumia karibu dakika thelathini, wakati huo ni karibu saa mbili.

¹⁹¹ Na toka saa mbili hadi saa tatu kasorobo, mahali fulani kati ya dakika thelathini na arobaini na tano, weka Neno hilo ndani mle jinsi tu Roho Mtakatifu atakavyokupea wewe (ona?), vivyo hivyo, liweke tu ndani mle jinsi Yeye asemavyo ufanye, ona, chini ya upako.

¹⁹² Ndipo toa wito wa madhabahuni, usema, “Je, kuna mtu ye yote katika kanisa hili ambaye angetaka kumkubali Kristo kama Mwokozi, tunawaulizeni ninyi, tunawaalikenii madhabahuni sasa hivi, simameni.” Ona?

¹⁹³ Na kama—na kama hakuna mtu anayesimama, sema, “Je, kuna mtu ye yote humu anayehitaji ubatizo, ambaye amekwisha kutubu, na anataka abatizwe kwa maji kwa ondoleo la dhambi? Kama wanataka kuja, tunawapa nafasi hii sasa, mwaweza kuja hali kinanda kinaimba.” Ona?

¹⁹⁴ Kama hakuna ye yote ajaye, sema basi, “Je, kuna ye yote humu ambaye ange... ambaye hajapokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu na angetaka kufanya hivyo usiku huu, angetutaka sisi tumwombe?” Vema, labda mtu fulani asimame, basi hebu watu miwili au watatu wawawekee mikono, wawaombee. Wapeleke moja kwa moja ndani ya moja ya vile vyumba, mtu fulani akiwa nao ndani mle, wafunze mahali fulani jinsi ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kusanyiko lote liko mbali nao.

¹⁹⁵ Kama mtu ye yote akija ku... ataka kumpokea Kristo na amesimama pale madhabahuni aombewe, fanya... hebu waombe. Na wakifanya hivyo, sema tu, “Inamisheni vichwa vyenu sasa, tutaomba.” Kisha sema, “Mnaamini?”

¹⁹⁶ Kama kuna jambo fulani ndogo ambalo huenda likawachelewesha waumini kwa njia iwayo yote, wapeleke kwenye chumba cha maombi, na uingie mle pamoja nao, au mtume mtu fulani mle pamoja nao. Kisha acha waumini waendele, ona, hivyo, hujawakawisha po pote basi. Ona?

197 Kisha wakati...kabla...Katika—katika dakika chache, unasema...Kama hakuna ye yote ajaye, basi sema, “Je, kuna ye yote ambaye angetaka kupakwa mafuta usiku huu, kwa ajili ya magonjwa? Sisi hapa huwaomba wagonjwa.”

198 “Vema ningetaka kukuona faraghani, Ndugu Neville.” “Vema, nione afisini. Ona mmoja wa mashemasi, watakushughulikia, ona.” “Na nina jambo fulani ambalo ningetaka kukwambia wewe, Ndugu. Vema, mmoja wa mashemasi hapa atakuleta afisini, nasi tuta...Nitakuona wewe mara tu baada ya ibada.”

199 “Sasa, tutasimama sasa tupate kupumukana.” Ona, na hamjakaa zaidi ya saa moja na dakika arobaini na tano katika mambo hayo yote. Ona? Ona, katika muda wa saa moja na dakika thelathini, ibada yenu imekwisha. Umepigilia kidogo, na upesi, ume—umetenda ilivyostahili; umetenda hayo na kila mtu ameridhika, na anaenda nyumbani akijisikia vizuri. Ona? Usipofanya hivyo basi, mwaona, ukiacha...Ona, u—u—Unakusudia mema, ona, lakini ona...

200 Mwajua hii ni karibu miaka thelathini na mitatu katika jukwaa hili kwangu, miaka thelathini na mitatu, na kote ulimwenguni. Unajifunza kitu fulani kidogo katika wakati kama huo, hakika. Ona? Usipojifunza, heri ujiuzuru. Kwa hivyo basi, ona, naona hili. Sasa, kama unashughulikia tu watakatifu wote pamoja, wee, ungeendelea usiku kucha kama ungetaka kufanya hivyo. Lakini una—...Ona, haushughulikii hao tu hasa, unajaribu kuwapata hawa nje hapa. Hawa hapa ndio unaowashika, yakupasa ufanye kazi kwao. Ona? Na usi...Walete humu kisha acha Neno lije, halafu, ona, hakuna cho chote ambacho chaweza kulalamikiwa. Kama wanataka kukuona kwa jambo lo lote, vema, sawa, wapeleke moja kwa moja hadi afisini hivyo, lakini usiwacheleweshe waumini.

201 Ndipo mwajua, watu watasimama na kusema, “Vema, na tuwe na mkutano mzuri wa ushuhuda.” Ona? Sasa, sikusudii kupinga hili, nakusudia tu kuwaambia ukweli. Ona? Nakusudia tu kuwaambia ukweli. Ona? Nimeona mikutano ya ushuhuda ambayo...hiyo—hiyo hudhuru kuliko inavyonufaisha. Ona, hiyo hufanya hivyo hakika.

202 Sasa, kama mtu fulani angekuwa na ushuhuda motomoto katika wakati wa ufufuo, mwajua, una ufufuo unaowaka moto, mwajua, mkutano, na mtu fulani aliokoka na anataka tu kusema neno, vema, Mungu abarikiwe, hebu basi aushushe mzigo wa nafsi yake. Kisha ona kama yeye...kama yeye ataka ku—kama yeye anataka kufanya hivyo, ona, katika tu wakati wa mkutano wa ufufuo, aseme, “Nataka kusema, ‘Namshukuru Bwana kwa yale Yeye amenitendea mimi.’ Yeye aliniokoa juma lililopita, na moyo wangu unawaka Moto kwa utukufu wa Mungu. Mungu

ashukuriwe,” aketi chini. Amina! Hilo ni zuri, endelea. Ona, hilo ni sawa.

²⁰³ Lakini usemapo, “Sasa basi. Nani anayefuata? Nani anayefuata? Sasa hebu na tusikie neno moja, na tusikie ushuhuda mdogo.” Sasa, kama mna mkutano uliotengwa, usiku fulani kwa hayo, ona, mtafanya hivyo. “Usiku huu . . . Jumatano ijayo usiku, badala ya mkutano wa maombi, itakuwa mkutano wa ushuhuda. Tunataka kila mtu aje, na utakuwa mkutano wa ushuhuda.” Ndiposa wajapo ma—mahali pale kutoa shuhuda, someni Neno, ombeni, kisha useme, “Sasa, tumetangaza huu kuwa usiku wa ushuhuda.” Kwa hivyo hebu watu washuhudie kwa muda wa saa moja au dakika arobaini na tano, au dakika thelathini, au zo zote zile, halafu—ndipo endeleeni hivyo. Mwafahamu ninalomaanisha? Nami nadhani itafaidi kusanyiko lenu, itafaidi kila kitu, kwa jumla, mkikiifanya hivyo.

²⁰⁴ Sasa, ninachelewa, kwa hivyo . . . Ndugu, ndugu zanguni, haya ni kadiri ni juavyo mimi. Naona yale yaliyo moyoni mwenu, haya ni kadiri ni juavyo katika maswali ambayo mumeuliza. Naam, tangu sasa mnajua. Na kama yakiwahi kuwa mawazoni mwenu, rudini kwenye kanda. Uliza hayo . . . Sikizeni kanda. Kama ni kwa ajili ya mashemasi, wadhamini, au ye yote yule, na kanda hii ichezwe. Na ichezwe waumini nje kule wakitaka kusikiza. Vema. Basi hayo—basi hayo ni kadiri ni juavyo mimi kuwa mapenzi ya Mungu kwa maskani haya hapa kwa Barabara ya Nane na Penn, na hivyo ndivyo ninavyowaagiza ninyi Ndugu kutekeleza haya chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, kwa wema wote na upendo, kuonyesha fadhili zenu mbele za watu kuwa ninyi ni Wakristo. Na Wakristo haimaanishi watoto wachanga ambao wanaweza kusukumwa po pote, hilo lamaanisha “Mtu aliyejawa na upendo, lakini ame—amejaa tu upendo kwa ajili ya Mungu kama vile yeye alivyojaa kwa ajili ya waumini.” Mwafahamu ninalokusudia?

²⁰⁵ Kuna swali? Kanda iko karibu kuishia hapa, nami nina mtu fulani anayeningoja pale. Yeye alikusudiwa kuwa hapo saa ngapi? [Billy Paul ajibu, “Sasa hivi.”—Mh.] Sasa hivi. Yeye anakuja peke yake? [Billy Paul ajibu, “Nitaenda kumleta.”—Mh.] Vema. Vema, bwana.

²⁰⁶ Sasa, najua tunaondoka nje sasa kama ha—hakuna tena neno lo lote. Sasa, kama sivyo, vema, na tupumukane. Naam, Ndugu Collins? [Ndugu Collins asema, “Ni heri kama kanda hii ingefungwa.”—Mh.] Vema. [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]

²⁰⁷ Vema, ndugu, nafurahia kuwa hapa pamoja nanyi usiku huu, na Ndugu Neville, na kwa mashemasi, na wadhamini, na msimamizi wa shule ya Jumapili, ninyi nyote. Tunatumaini kuwa Bwana atawasaidia ninyi sasa kutekeleza taratibu hizi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sababu ya kusema haya ni kwa sababu nafikiri mmekua kutoka watoto hata watu wazimu.

Mlipokuwa watoto, mlinena kama watoto, na mlifahamu kama watoto. Lakini sasa ninyi ni wanaume, kwa hivyo na tutende kama watu wazima katika nyumba ya Mungu, tukijiadibisha wenyewe, na kuheshimu afisi zetu, na kuheshimu kila afisi. Kila karama ambayo Bwana ametupea, na tuviweke katika taratibu, na kumheshimu Mungu kwa karama zetu na afisi zetu.

Na tuombe:

²⁰⁸ Baba uliye Mbinguni, tunakushukuru Wewe usiku huu kwa ajili ya huku kukusanyika pamoja kwa watu waliowekwa katika afisi hapa kutekeleza kazi ya Bwana inayofanywa hapa katika Jeffersonville katika kanisa hili. Mungu, na mkono Wako uwe juu yao, wasaidie na kuwabariki. Na waumini na watu hawa wafahamu na kujua kuwa hili ni la kustawisha Ufalme wa Mungu, kusudi tuwe watu wanaofahamu na kujua Roho wa Mungu, na kujua la kufanya. Tujalie, Baba. Turuhusu tuende sasa na baraka Zako, na Roho Mtakatifu atuchunge na kutuongoza, na kutulinda, na tupatikane daima waaminifu kazini mwetu. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba. Amina. 

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org